KARAMA ZA MUNGU DAIMA HUPATA MAHALI PAO

Asante, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, "Mungu akubariki, ndugu."—Mh.] Bwana akubariki, ndugu.

Habari za jioni, marafiki. Ndiyo kwanza niingie, muda mfupi uliopita, na niliwazia ningeweza kuteremka huku niwatakieni nyote "Heri za Krismasi."

2 Basi kwa hiyo sikujua kwamba ningekuwa na majaliwa haya makuu kuwazungumzia juu ya Neno la Bwana. Na kwa hiyo Ndugu Neville aliniomba, nami nilikuwa na mafungu madogo kadhaa ya Krismasi ambayo nimekuwa nikitumia, moja ya hayo huko katika—katika Phoenix na huko chini Tucson, sehemu mbalimbali kule, ujumbe wa kawaida wa Krismasi. Ndipo nikawazia, usiku wa leo, ningenena tu juu ya kitu kidogo hapa ambacho Bwana aliweka mawazoni mwangu hivi majuzi, nilipokuwa huko juu Colorado.

3 Na mimi nilikuwa nikiwazia juu ya jambo fulani kwenye wakati wa Krismasi, ndipo nikapata yapata kumbukumbu tano au sita nilizoandika hapa, Maandiko na kadhalika. Ninii . . . sininii . . . Nadhani Ndugu Neville na wahudumu wote hufanya hivyo. Wewe . . . inaonekana kana kwamba jambo fulani linakujia, nawe unaliandika. Unasubiri kidogo, halafu unaliandika. Ninaliweka kwenye kijipande cha karatasi, kwenye kijipande tu cha karatasi. Ndipo ninapoitwa wakati fulani, nitaangalia nyuma kupitia hapa na kusema, "Hii ilikuwa ni nini sasa ambayo niliishika?" Hiyo ndiyo njia, tunapoitwa haraka sana, mnajua.

4 Ilikuwa kwamba, mimi . . . wakati nilipokuwa mdogo zaidi, ningeweza tu . . . akili yangu ilikuwa kwamba, ningeweza tu kuwazia hili sasa hivi, na haikunibidi kungojea, nafikiri "Siku kumi zilizopita nilikuwa mahali fulani, fulani. Hilo ndilo fungu. Hili hapa, na hapa linaenda."

5 Unajua, kwa vile nimepita hatua chache, Ndugu Higginbotham, na kuvuka mito michache, kwamba haiji hivyo tena, nikifikia mbali kidogo kwenye barabara. Lakini hiyo . . . kama Ndugu Neville alivyosema, muda mfupi uliopita, "Tunakaribia Nyumbani zaidi, zaidi."

6 Ni vyema kurudi nyumbani. Mimi, ninarudi, mbona, kuna theluji nyingi sana. Na kuna . . . na kusikia kuhusu ajali na kadhalika, nyingi sana barabarani, na watu wanauawa. Pia wazia tu ni mamia mangapi watakaopoteza maisha yao sasa, kati ya usiku wa leo na baada ya ule wa Mwaka Mpya, ni

Wamarekani wangapi watakaofariki! Tena unajua, baadhi yetu huenda tukawa papa hapa, usiku wa leo. Na inategemea tu sasa, kwamba. . .hali yetu mbele za Mungu. Ni taifa lenye huzuni, ndugu huyu alisema, huzuni kila mahali. Na bendera yetu imekuwa ikining'inia, siku thelathini, nusu mlingoti, yote kwa sababu ya dhambi na watu ambao wasingepokea njia ya Mungu ya—ya—ya mambo.

7 Hata kama tunaweza kukosa kukubaliana na mtu, ikiwa hatuwezi hata hivyo kuifanya kwa njia ya udugu, na halafu. . . Mnaona, kama Kristo yuko moyoni, basi haijalishi ni kiasi gani mmekosa kukubaliana na mtu huyo, ungali unampenda na kumheshimu. Sikubaliani na watu wengi, mara nyingi. Lakini hata hivyo, bado sijawahi kumwona mmoja niliyekosa kukubaliana naye ambaye nimemwazia zaidi ya "kumkumbatia na kumwita 'ndugu yangu,' nijaribu kumsaidia kadiri niwezavyo." Sikubaliani na yeye kwa sababu kwamba nafikiri labda kwamba juu ya kutokubaliana kwamba yeye. . .Kile anachoamini, kwamba huenda nisiamini tu kama yeye, bali. . . na kadhalika, lakini sasa huenda nikajaribu kumwonyesha njia yangu huku akinionyesha yake, na kuziweka pamoja na kuchambua na kuona tulicho nacho, lakini kutokubaliana namna hiyo. Kama tu inavyofikia kwenye. . .hatupaswi kukasirika wala kutaka kudhuru, au kuangamiza au chochote. Daima tunapaswa kuwa tukijaribu kujenga.

8 Tuna kipindi cha baridi kinachoendelea hapa, sivyo? Sabini na mbili nilipotoka Tucson, na wakati jua lilipotua na kukawa giza, ilikuwa ingali sitini na tisa. Kwa hiyo, basi kurudi hapa juu, ninatetemeka kabisa, mwajua. Mimi. . .Barabara hiyo iliyojaa theluji, na chini ya sufuri, na barafu na kila kitu, ilinibidi kuizoea tena. Ni ajabu sana jinsi unavyoweza "kuzoea hali ya nchi" katika njia ndo—ndogo hivyo. Na tangu nilipoondoka, karibu sikuwa na nafasi ya kustahimili. Ninayo. . .kama mapindi katika ha—hali ya anga hapa ndani, na ninavyozidi kuzeeka. . .Nami nilizaliwa na kukuzwa hapa ndani. Lakini wakati, unaona, unapokuwa mdogo, una kitu fulani, unaweza kukitupa; bali unapokuwa mkubwa, mbona, unaanza kugundua kwamba kitu fulani hakipo. Ilikuwa kwamba, ungeweza tu kusahau hicho. Wewe. . .kuna kitu hapo ambacho—ambacho hakitatupa tu kama kilivyofanya ulipokuwa mtoto, kwa hiyo ninabaini hivyo kwamba mimi. . .hali hiyo ya joto, kwa mtu mzee, kwa namna fulani husaidia kidogo.

9 Ninakumbuka kuteremka ile Barabara ya Utica pale juu, kama mtoto (umri wa miaka saba, nane, kumi, kumi na mbili, kumi na minne), bila viatu mguuni (viatu vya raba) na ni nane au kumi chini ya sufuri, na viatu vya raba, vidole vimejitokeza nje. Na si. . .sasa huko si kutembea kuteremka kama barabarani hapa, bali ni kupenya theluji. Hakuna motokaa zinazoteremka, huenda kukawa na mkokoteni mara moja moja.

Teremka kwenye barabara hiyo kuu asubuhi, umevaa maskini koti dogo, bila shati, nalo limefungwa juu namna *hii*, si zaidi ya kile nilichovalia sasa; unyevu wa kulowesha kufikia magotini mwangu, unaendelea moja kwa moja bila kuyajali hayo. Unaona, ni nadra sana kuwa na mafua. Bali hiyo ilikuwa ni yapata miaka arobaini na tano iliyopita. Kwa hiyo, kudhoofika kwingi, nimeenda maili nyingi na kuongezea kwenye kipima spidi, mwajua, kwa hiyo hatuichukui tu jinsi tulivyozoea kufanya.

10 Nilimwona Ndugu Capps akiinua kichwa chake. Wewe ni mdogo sana kuwazia mawazo hayo sasa. Basi kwa hiyo ngojea mpaka ufikie mahali tumefikia mimi na Ndugu Neville, ndipo—ndipo uta—utawazia mambo mengi vinginevyo, kwa namna fulani hudhoofisha.

11 Vema, tumekuwa na nyakati adhimu katika Bwana. Bwana ametubariki sana, nami ninashukuru sana. Na ninarudi, nafikiri, Jumapili ijayo, Bwana akipenda, ninataka, ikiwa Ndugu Neville hatajali, ninii. . .Nina ibada, angalau Jumapili asubuhi na labda Jumapili usiku, ibada ya uponyaji kwa ajili ya Jumapili usiku. Jumapili asubuhi ninao ujumbe muhimu, kama Bwana akipenda ili niweze kuutoa. Sijaliwaza fungu langu. . .si zaidi tu ya fungu langu bado, halina muktadha, kwa sababu mimi—mimi. . .si pasipo—pasipo wowote, mnajua, ufunuo kutoka kwa Bwana, ila tu ndani yangu. Na—nataka kueleza jambo fulani Jumapili ambalo ninatumaini kwa namna fulani litasaidia kidogo katika njia hizi.

12 Inanibidi sasa kwenda hudumani, na karibu kila siku niliyo nayo imechukuliwa kila mahali. Nafikiri Billy alikuwa akiniambia, katika utaratibu wa safari, kwamba nina siku mbili ama tatu ambazo ningeweza kuja nyumbani katika Aprili baada ya kuondoka hapa, kurudi Tucson, na hiyo karibu inaimaliza basi. Halafu basi kuendelea mpaka Novemba ijayo, Oktoba, nitakaporudi huku tena kutoka ng'ambo.

13 Sasa, siku mbili zaidi kufikia Krismasi. Siku moja zaidi, sivyo? Hizo zingekuwa mbili. Jumatatu. . .Jumanne ni mkesha wa Krismasi? Jumanne ni mkesha wa Krismasi. Si ni vibaya sana kuona kwamba hii sikukuu muhimu, tunayoikaribia, inakaribiwa kwa njia inayokaribiwa? Ni kitu cha kusikitisha mno, kitu cha ki—ki—kijinga sana, kuwazia kwamba—kwamba sungura na ha—hadithi ya uongo inayoitwa "Kriss Kringle" (Baba Krismasi) na kila kitu, vimeondolea mbali thamani ya kweli kutoka kwa kile Krismasi ilicho.

14 Sasa, sisi hatuninii. . .sisi—sisi hatujui, na hakika siamini. . .Nilikuwa tu nikishuka kuja, mke wake yuko pale nyuma, na mimi. . .tukishuka kuja barabarani, tulikuwa tukimsikiliza mnajimu; ambao sasa, waliangukia tu wazo ambalo mnajimu mmoja aliniambia miaka mingi, mingi iliyopita, nilipokuwa tu bwana nyama hapa Indiana.

Waliponiambia kwamba . . . jinsi hizo nyota zilivyokutana, kama tu yule mnajimu wa kwanza alivyofanya na hiyo ilitengeneza, kile ambacho walisema kingekuwa kitu cha kimaumbile ambacho hutendeka kila, naamini alisema usiku wa leo, miaka mia nane, ama kitu kama hicho. Na hiyo hujirekebisha tena, wa: Sargas na Jupiter, na ninasahau; na Mart- . . . Mars; hapana, mimi . . . hilo ni kosa. Ni baadhi ya nyota jinsi zinavyoenda kasi zinapopitia kwenye mizingo yao katika mzingo wa dunia, naye mnajimu huyu usiku wa leo alikuwa akijaribu kusema kwamba kwa kweli lilikuwa ni jambo la kimaumbile. Si—sininii—silikubali hilo. Ninaamini lilikuwa ni jambo la kimbinguni, ambalo Mungu alitenda. Yeye, mambo ni ya kimbinguni na Mungu. Yeye ni wa Kimbinguni.

15 Ndipo—ndipo nikaangalia chini na kujua kwamba hii inatazamia nyuma sasa kwenye Aprili, nimeninii . . . Bwana akipenda ili niishi muda mrefu hivyo, nitakuwa na umri wa miaka hamsini na mitano. Mnaona? Nami na—najua ninii . . . Bali nikiangalia nyuma katika maisha yangu, na ninashangaa ni wapi lilipotokea. Kuanzia maskini Krismasi za mwanzoni, wakati tuliponing'iniza soksi zetu, na Mama angechukua . . . Labda tungechukua chungwa, na vipande viwili au vitatu vya peremende yenye milia, na hiyo ilikuwa ni Krismasi kubwa kwetu. Lakini, unajua, watoto wao—wao hutazamia zawadi. Tu—tunaona ya kwamba—kwamba Krismasi ni kwa . . . sana sana ni watoto, wao—wao huitazamia hiyo siku hizi. I—imewageukia watoto. Bali kwa kweli inafaa iwe ni watu wazima; inapaswa kuwa kufundisha watoto wao kile ilicho Krismasi halisi.

16 Nami siamini kabisa kwamba—kwamba Kristo angeweza kuzaliwa kwenye tarehe ishirini na tano ya Desemba, huko Uyahudi, kwa sababu ni baridi kuliko ilivyo hapa sasa. Mnaona? Loo, na wachungaji wangewezaje kuwa wakichunga kondoo wao usiku? Halafu—halafu kutozwa ushuru na kila kitu, naye Mariamu kulazimika kuja umbali huo, kutoka huko chini Bethlehemu kupanda kuingia Judea, kupanda kuingia Yerusalemu, hasa, kwenye ninii . . . kwa ajili ya kulipa ushuru. I—i—ingekuwa vigumu kwangu kuweza—kuweza—kuweza kuamini hilo. Kupanda juu, naamini alikuja Nazareti, na kwa hiyo wakati . . . Jinsi hilo—hilo lingeweza kutendeka. Isingeweza ku—kufanywa, bali ninaamini kwamba Kristo alizaliwa kwenye majira ya kuchipua, kwa sababu kwa kila njia Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo. Mnaona? Mnaona, Yeye alizaliwa katika zizi, na si nyumba?

17 Basi walipompeleka msalabani (wengine), kama tujuavyo, kwamba hakusema kuhusu Yeye kuwaongoza, bali wao walimwongoza. Je! ulijua kwamba mwana-kondoo ama kondoo hana budi kuongozwa kwenda machinjioni? Ha—hataenda machinjioni, i—inakubidi kumwongoza huko. Na

kwa kawaida ni mbuzi ndiye huongoza kondoo. Katika—katika vizimba vya kuchinjia, wana mbuzi. Naye mbuzi atatembea kwenye njia hii, mpaka atakapofikia kumfanya kondoo aanze kuitembelea njia hii apate kuuawa, ndipo basi mbuzi ataruka nje. Lakini ukiwadia wakati wanapoenda kumwua mbuzi, yeye analeta fujo kwelikweli (hana budi kuingia) lakini, hakika, usingeweza kumlaumu. Bali—bali ni ja—jambo kubwa jinsi kondoo hana budi kuongozwa, na Yeye aliongozwa hadi machinjioni. Walimwongoza. Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo. Nami ninaamini katika njia hiyo kuwa ni maumbile kabisa, na wana-kondoo wanazaliwa Machi, Aprili, na mahali fulani karibu hapo, si mbali zaidi ya Mei. Wala siamini kwamba ilikuwa ni chochote kabla ya Machi na chochote baada ya Mei, wakati fulani karibu hapo.

18 Bali wakati kanisa, Ukristo, ulipoingizwa katika Urumi, ilikuwa ni kwenye Baraza la Nikea, wakati walipokubali . . . taifa la Kirumi lilikubali Ukristo na kuunda kile walichokiita dini ya watu wote, ilikuwa ni Ukristo. Waliunda dini ya watu wote, na wakaabudu sanamu, nao walikuwa na mungu-jua.

19 Basi sasa hivi, kuanzia tarehe—kuanzia tarehe ishirini na moja hadi ishirini na tano, jua karibu husimama katika mkondo wake ule ule linapopita. Mnaitaje hiyo? Imekuwa ninii . . . Nilidhani niliijua, lakini siwezi kuikumbuka. Wakati jua ni—ni . . . hu—huongeza muda kiasi na kupoteza muda kiasi, mpaka tarehe ishirini na moja, kati ya tarehe ishirini na moja na ishirini na tano ya Desemba. Loo, ninasahau wanavyoita hiyo. Nini? [Mtu fulani katika kusanyiko anasema, "Kupatwa jua?"—Mh.] La, kupatwa jua ni wakati linapopita, jua na mwezi hupita kwa pamoja. Ni kitu fulani hapo, loo, ka—ka—karibu ninaweza kulitamka bali siwezi sasa hivi. Hata hivyo, ni kusimama kimya kwa jua ambako kunaitwa na Warumi (hapo ni wakati sarakasi zilipofanyika), kuliitwa *siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua*. Waliisherehekea hiyo kuanzia tarehe ishirini na moja hadi ishirini na tano Desemba.

20 Kwa hiyo basi, kwa kuwa hii ilibadilishwa, Roma ikawa . . . Ukristo ulikubalika, kwa njia yao huko Rumi, basi wakasema, "Tutaifanya sherehe ile ile, na kufanya *siku ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu*." Mnaona? Mungu-jua, siku ya kuzaliwa kwa Jupita, halafu siku ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu, tarehe ishirini na tano Desemba, na hiyo . . .

21 Lakini inaleta tofauti gani? Mnaona, leo hii wakati sisi . . . Hata kama ni ninii . . . kama walikuwa wakiifanya Julai ama Agosti, ama wakati wowote hiyo ingekuwa, ingali ni utakatifu wa kukumbuka kwamba "Mungu alitupatia tumaini tulilo nalo ndani yetu."

22 Na sasa, unasema, "Vema, yote yaliyosalia ni Baba Krismasi na kuendelea kama wafanyavyo; mbona, tunaweza tu kufanya

hayo hata hivyo.” La, bwana! La, hii si sherehe ya kipagani kwetu sisi, haya ni majira ya kicho. Kama kusingekuwa na Krismasi, kusingekuwa na ufufuo. Kama kusingekuwa na Krismasi: kusingekuwa na upendo, kusingekuwa na amani, kusingekuwa na maisha ya baadaye kwa mwaminio; kama kusingekuwa na Krismasi.

23 Basi sasa, unasema, “Vema, kama ulimwengu wote, wananinii tu. . . ” Vema, unaona, radi iliyogawanyika kwenye anga zenye giza, na mawingu, inaonyesha kwamba kunaweza kuwa na nuru wakati wa giza. Taa hizi usiku wa leo zinathibitisha hilo, kwamba kunaweza kuwa na nuru wakati wa giza. Na ni wakati gani nuru huangaza vizuri zaidi? Katika giza. Ukiwasha taa hizi wakati wa mchana, jua linaangaza ndani, itakuwa vigumu kutambua kuwa zinawaka. Bali maskini taa moja, ndogo sana itawaka angavu sana kwenye wakati wa giza. Na sasa hivi ni giza wakati kila Mkristo anapaswa kutoa ushuhuda wa tumaini lililoko ndani yake, wa Yesu Kristo Mwana wa Mungu; si Kriss Kringle fulani aliyezaliwa huko nyuma, mwajua, na namna fulani ya mti uliowekewa taa na kuteremka kupitia msituni usiku mmoja, hadithi fulani ya uongo ambayo haina msingi. Bali tunaamini kwa dhati juu ya Neno la Mungu lililoahidiwa la Masihi ajaye, na Yeye alizaliwa kwenye siku ya Krismasi, ishirini. . .karibu miaka elfu mbili iliyopita, tunaamini.

24 Kwa hiyo, usiku wa leo tunaenda kuzungumza kidogo kwa njia tofauti. Nadhani mchungaji wenu tayari amehubiri, na labda atahubiri Jumatano usiku tena maana na—najua aliweka kando fungu fulani ama kitu kama hicho, kunipa mimbara hii usiku wa leo. Nami ninamtaka alete hilo, ninataka kumsikiliza.

Lakini, kabla tu hatujafanya hili sasa, hebu tuinamishe vichwa vyetu tena kwa muda mfupi wa maombi:

25 Baba wa Mbinguni, wakati huu mkuu wenye kicho, tunapowazia mambo mbalimbali katika Maandiko hapa, kwamba popote tuendapo, nyuma katika Agano la Kale, inazungumzia siku ile ambapo Mungu atamtuma Mwana Wake. Jinsi ambavyo wale manabii huko nyuma walichukua wakati wao ili unabii wa Neno la Mungu uwajie. Nao walitabiri katika siku zao na kunena kimbele mambo ambayo yangekuja kutimia, na tunaona yote yalikutanika kule Bethlehemu usiku ule wakati Mungu aliupenda sana ulimwengu hata akamtoa Mwana Wake wa pekee. Tunakushukuru Wewe kwa hili.

26 Pia sasa, Bwana, usiku wa leo tunapotulia hapa ku—kuzungumza juu ya Neno Lako; na Hilo ni takatifu sana, Bwana, hiyo ndiyo sababu tunapenda kuzungumza na Wewe kwanza. Basi tunaomba ya kwamba Wewe utafungua ufahamu wetu kwa Neno Lako. Katika Jina la Yesu tumeomba hayo. Amina.

27 Sasa ninataka kusoma Maandiko fulani hapa, hadithi tu ya kawaida ya Krismasi, kwa Maandiko yanayopatikana katika—katika Mathayo, mlango wa pili. Na wakati mkifungua hilo, na Yohana 3:16.

28 Na hivi majuzi usiku huko Phoenix . . . Kama nyinyi watu wa kanda hapa, mnaosikiliza kanda, ningewatakeni msikilize huo: *Ni Kwa Nini Ilibidi Yesu Kuja Bethlehemu*. Ni kwa nini ilimbidi kufanya hivyo? Na mifano ile pale ya Daudi, akilala na—na kungojea juu ya mlima, akitazama chini na kuona jeshi la Wafilisti limezunguka. Nami nililinganisha hilo na leo hii hasa, na kuona kwamba Bethlehemu . . . inayomaanisha.

29 Naye Kristo ndiye Bethlehemu yetu, na ningeweza kuthibitisha kwamba kila mtu aliyezaliwa na Mungu amezaliwa Bethlehemu, maana Kristo ni Bethlehemu. Na hicho ndicho Yeye alichokuwa, *Mkate wa Uzima*. Basi Beth, *B-e-t-h* maana yake—maana yake “nyumba,” *E-l* ni “Mungu,” na e-l-h-e-m ni *Elhem* ambalo linamaanisha “mkate,” na “Nyumba ya Mkate wa Mungu.” Na Yesu Kristo alikuwa ndiye “Nyumba ya Mkate wa Mungu,” Mkate wa Uzima wa Milele. Basi kila mtu aliyezaliwa ndani ya Kristo, umezaliwa ndani ya *Bethlehemu*, “Nyumba ya Mungu ya Mkate.” Na jinsi ambavyo mashirika ya makanisa haya leo yamezungukwa, kama Wafilisti, kuwazuia watu wasiendee Hilo.

30 Na jinsi ambavyo watu wale hodari, wakijua kwamba Daudi alikuwa ametiwa upako na alikuwa anaenda kuwa mfalme siku moja . . . asiyependwa sana na wengi wakati huo, kwa sababu alikuwa mtoro miongoni mwa watu wake, lakini siku moja wito wake ukaja. Walikuwa na watu hodari pamoja naye. Tena kumbuka, watu hao walikuwa Wamataifa, karibu kila mmoja wao walikuwa Wamataifa, mfano mzuri sana wa leo hii. Basi mtu mmoja alikuwa shujaa sana, aliwaua watu mia nane kwa ninii . . . kwa mkuki wake, mwenyewe, katika siku moja. Mwingine alikuwa amesimama katika shamba la dengu, ndipo jeshi likaja, kikosi. Na wote wakakimbia, naye akasimama hapo na kuwaua watu mpaka mikono yake ikachoka. Ndipo basi mwingine, jinsi alivyoruka kwenye shimo na kumwua simba kwenye siku yenye theluji, peke yake. Ndipo Mfilis- . . . ama Mmisri akamkimbilia, akiwa na mkuki mrefu, naye akachukua fimbo na kuupiga mkuki huu ukatoka mkononi mwake, akachukua mkuki huo na kumwua Mmisri mwenyewe, na kuwaua makapteni mia tatu.

31 Na akatoa watu mashuhuri! Daudi akilia, “Laiti ningalikunywa mara moja zaidi, unaona, kutoka kwenye kile kisima!” (ambapo alikuwa akiwanywesha kondoo wake alipotoka asubuhi, kutoka zizini, wangetaka maji ya kunywa) Basi watu hawa wakachomoa panga zao na kupiga vita kupitia kwenye watu maili kumi na tano, wakaleta maji haya.

32 Ndipo Daudi akasema, "Na iwe mbali, kwamba nitayanywa." Basi akayamwaga juu ya nchi kama sadaka ya kinywaji kwa Bwana. Ni mfano mzuri jinsi gani wa kitu kile kile, wa hii Yohana 3:16, usiku wa leo.

> *. . .Mungu aliupenda sana ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, . . .*

33 Basi Kristo alifanya nini? Ule Uhai aliokuwa nao kuishi Milele, Yeye aliumwaga juu ya nchi kutoka kwa vena Zake, uhai Wake wa kawaida, juu ya nchi kama toleo la dhambi kwa ajili yetu. Na vile Wamataifa leo hii, watu wa heshima, wanaume, wanaume mashuhuri, wakichukua upanga, na kusimama pale na kupenya ili kumletea Kristo (Daudi wetu) maji safi ya kunywa, ambayo hayapendwi na wengi leo hii. Bali Daudi wetu, ambalo tunajua Yeye anakuja mamlakani, Yeye anaenda kukanyaga kila taifa chini ya miguu Yake namna hiyo, na kuwatawala kwa fimbo ya chuma. Na watu hodari kwelikweli, wakisimama na Neno la Mungu na kukata kutoka upande mmoja hadi mwingine bila woga, maana tunajua Yeye anakuja mamlakani.

34 Hebu tusome sasa, baada ya Yohana 3:16; hebu tusome ile ziara ya—ya wale Mamajusi wa Mathayo Mtakatifu, mlango wa pili.

> *Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama mamajusi wa—wa mashariki walifika Yerusalemu,*
>
> *Wakisema, Yuko wapi yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia.*
>
> *Basi mfalme Herode. . .aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye.*
>
> *Akakusanya. . .wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta habari kwao, Kristo azaliwa wapi?*
>
> *Nao wakamwambia,* Katika *Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii,*
>
> *Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda, hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda;. . .kwako atatoka Mtawala, atakayewachunga watu wangu Israeli.*
>
> *. . .Herode akawaita wale mamajusi faraghani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota.*
>
> *Akawapeleka Bethlehemu, akasema, Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie.*
>
> *Nao. . .waliposikia maneno ya mfalme, walishika njia; na tazama, ile nyota waliyoiona mashariki*

ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto.

Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno.

Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao . . . walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu . . . uvumba, na manemane.

Nao wakisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasiondoke . . . *wasimrudie Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.*

35 Ni ajabu sana hapa jinsi ambavyo Mungu, katika njia duni, . . . Mungu huwanenea watu kupitia ndoto. Ninaamini hilo. Lakini jinsi ambavyo Mungu katika kisa hiki alitumia njia ya pili.

36 Sasa, ndoto ni . . . ndoto, ikitafsiriwa vizuri, ni sawa na ono; ikiwa ni ndoto na inatafsiriwa. Mungu ameitumia tangu huko nyuma katika Agano la Kale na kote kupitia nyakati, na kuahidi katika siku za mwisho kuitumia tena. Sasa, watu wanaweza kula kupita kiasi na—na kadhalika na kupata jinamizi, na siyo—siyo ndoto halisi, za kiroho, haipigi kengele wakati unaponinii—wakati unapoisoma. Na baadhi yake huenda zikaonekana sahihi, bali kuna ndoto halisi, za kiroho. Nasi tunajua hapa kwenye maskani kwamba Mungu huwapa watu ndoto nazo zinatafsiriwa, na zinatimia, nazo ni halisi. Bali ni njia ya pili ya kufanya hivyo. Unaona?

37 Sasa, sababu ya hiyo kufanywa wakati huo, ilikuwa ni kwa sababu hakukuwako na nabii nchini wakati huo, kuitafsiri ndoto. Unaona? Hakukuwako na nabii kuzifasiri ndoto, kama vile Yusufu na—na Danieli na wale manabii wa kale. Hawakuwa wamekuwa na nabii kwa miaka mia nne, na Mungu alitumia ndoto kuninii . . . kwa manufaa ya Mtoto Wake Mwenyewe. Alitumia.

38 Alimwambia Yusufu, wakati alipokuwa "mtu mwenye haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri." Hapana shaka alimwambia kuhusu kuzuriwa na Gabrieli na kadhalika, na kile alichokuwa amesema; lakini alipomwona akiwa mja mzito, li—lilikuwa ni jambo geni kabisa. Mnajua, ilininii tu . . . lilikuwa ni jambo tofauti kabisa. Basi mnajua, hiyo ndiyo shida leo hii. Mungu hufanya mambo kwa njia isiyo kawaida, na si kawaida kabisa mpaka hata mtu mwenye haki hawezi kuliona.

39 Yusufu asingeweza kuelewa hilo, lilikuwa lisilo la kawaida kabisa. Alikuwa ni mtu mwema, hana ubaya wowote. Alikuwa ni mtu mwema, mtu mwenye haki, bali lilikuwa lisilo la kawaida sana. Unaona, Yusufu labda akiwa na umri wa miaka arobaini ama arobaini na tano, kitu kama hicho, wanadai, wakati yeye na Mariamu walipoposana. Lakini hapa tunapata jambo ambalo

halikuwa limetukia: mwanamke aliyeposwa na mume huyu na hata hivyo apatikane kuwa na mimba! Na lilikuwa jambo lisilo la kawaida sana hata Yusufu alikusudia kumwacha. Bali moja kwa moja kwenye wakati huo muhimu sana, Mungu alimtuma Malaika Wake, na akamtokea katika ndoto na kusema, "Usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana Mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu."

40 Ni imani mpya ya jinsi gani iliyozaliwa ambayo hapana shaka Yusufu alikuwa nayo alipoamka kutoka hapo! Unaona, kamwe hakuhitaji tafsiri yoyote, ndoto hiyo haikuwa katika mifano. Ilikuwa ya moja kwa moja, "Usihofu kumchukua Mariamu mkeo, kwa kuwa Mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu." Hakukuwa na nabii wa kutoa tafsiri, kwa hiyo ilibidi ije moja kwa moja, moja kwa moja wazi namna hiyo; kwa Mungu . . . kutoka kwa Mungu kumjia Yusufu. Sasa . . . na Mungu alichukua njia hiyo ya pili.

41 Inatufunza nini papa hapa, kabla hatujalifikia somo letu? Hiki hapa kile inachotufundisha: kwamba Mungu anaweza kutumia kila kipaji cha utu wetu kama ukikabidhi- . . . ukisalimishwa Kwake. Anaweza kutumia nia yetu, ndoto zetu, dhamira yetu ya ndani, dhamira yetu ya kwanza, ulimi wetu, nyimbo zetu, macho yetu, ninii yetu . . . Kila kitu tulicho nacho kinaweza kutumiwa na Mungu kikikabidhiwa kwa Mungu. Unaona? Kila kitu ulicho, kikabidhi kwa Mungu. Yeye atatumia kila njia na kila sehemu yako, Yeye ataitumia. Haijalishi ni nini, Yeye ataitumia iwapo imetakaswa kwa kusudi Lake na wito.

42 Sasa, usiku wa leo tunaenda kuzungumza juu ya: *Karama*. Nami ninataka kuupa huu kichwa, ikiwa . . . Niliandika, niliandika kitu fulani hapo ndani, wakati Ndugu Neville alipokuwa amesimama: *Karama Za Mungu Huwa Daima Hupata . . . Karama Za Mungu Daima Hupata Mahali Pao*. Karama za Mungu daima hukataliwa, bali kwa kweli hupata mahali pake wakati . . .

43 Sasa, angalia zawadi ambayo mamajusi hawa walinunua . . . ama walileta Kwake. Leo hii tunapata kwamba tunabadilishana zawadi. Kila mtu hana budi kupokea zawadi, na kujaribu kuwazia kile ambacho huyo jamaa mwingine anaenda kumpa, ili aweze kumpatia kitu akilinganisha hivyo. Na kama sivyo, vema, kwenye Mwaka Mpya, anahisi kwamba hana budi kuitimiza. Na kila mtu akichunguza na kufadhaika na kutembea sakafuni, mamilionea, jinsi watakavyofanya. Wanatoa kiasi fulani kwa *huyu* na *yule*, wakati yo—yote ni makosa. Yo—yo—yo—yote . . . Krismasi . . .

44 Hapa: ipo zawadi moja tu uwezayo kutoa, na hiyo ni wewe mwenyewe. Jitoe mwenyewe kwa Mungu kwa sababu Mungu tayari amekupa Karama Yake. Sasa, hicho hapo kitu pekee unachodaiwa na Mungu, hicho ni wewe mwenyewe Kwake.

45 Sasa, na mara nyingi, *majina* yako katika Biblia. Hatuitambui tena, leo hii. Sisi. . .Mara nyingi mmenisikia nikilibeza jina hili, la watoto kuita . . . ama watu kuwaita watoto wao "Ricky." Sasa, *Ricky* ni jina la kuchukiza! Unaona? Na ni. . .hampaswi kuwaita hivyo. Kama una mtoto anayeitwa Ricky, kwa hisani, libadilishe kuwa kitu kingine. *Ricky*, ama—ama *Elvis*, ama kitu kama hicho. . .*Ricky* maana yake "panya." Unaona? Na kwa hiyo u—unaenda. . .Na—na kile unachomwita mtu, hicho kinaathiri hiyo. Maskini mama fulani, hivi majuzi, alikuwa na mvulana mdogo huko nje aliyeitwa "Ricky" na jina lake ni Ricky, James Ricky. Na kwa sababu lilikuwa maarufu sana (Ricky), walimwita "Ricky." Nikasema, "Libadilishe jina hilo!"

46 Ninawaona watu wengine walioketi papa hapa sasa walio na mjukuu mdogo, na jina lake ni. . .yule—yule mvulana ni jamaa mwema, wa kupendeza sana; na yule mwingine ni Ricky, na hivyo ndivyo alivyo. Wewe mwangalie tu, tabia yake ni hivyo tu. Na yeye. . .Niliwaambia baadhi ya babu zake, ama mtu mwingine, nikasema, "Mwambie mama yake abadilishe jina la mvulana huyo, libadilishe tu hilo jina kabisa na uangalie kinachofanyika kwa mtoto huyo." Mnaona, nyinyi watu hamtaki kuamini hilo. Tunafikiri tumeishi muda mrefu sana kwa hilo.

47 Iwapo hakuna kitu katika jina, basi ni kwa nini mradi Yakobo aliitwa *Yakobo*, linalomaanisha "mwongo, mdanganyifu," hicho ndicho alichokuwa? Bali wakati alipomenyana na Bwana usiku kucha, na Bwana akabadilisha jina lake, na yapata. . .wakati alipokuwa na yapata umri wa miaka sitini. Alibadilisha jina lake kutoka—kutoka—kutoka Yakobo likawa *Israeli*, "mfalme mbele za Mungu," na hicho ndicho alichokuwa.

Ni kwa nini Abramu aliitwa. . .ilibidi aitwe "Ibrahimu" kabla ya mtoto kuweza kuzaliwa? Ni kwa nini Sarai akaitwa "Sara" kabla ya mtoto kuweza kuzaliwa?

Ni kwa nini Paulo. . .ama kuita. . .jina lake lilikuwa Sauli, lakini wakati alipokutana na Yesu, Yeye alimbadilisha kutoka Sauli akawa "Paulo."

Wakati Simoni alipobadilishwa kutoka Simoni akawa *Petro*, ambalo linamaanisha "jiwe dogo." Na—na majina yao yote yalibadilishwa, ni kwa sababu kile unachoitwa ni jambo fulani kukihusu. Unapozungumza jambo fulani, hujitambulisha lenyewe. Sitaki kuingia huko, maana hiyo inakuja Jumapili ijayo usiku, unaona, kitambulishi cha neno. Na, bali sasa, tunaona mambo haya ni kweli kabisa.

48 Sasa angalieni, Mungu. . .Ni kitu cha kigeni jinsi gani usiku wa leo, kuona kwamba watu hao, Mamajusi, watu wenye elimu, watu mashuhuri . . . wakiteremka kutoka Mashariki, hiyo ilikuwa ni Babeli, ambayo ilikuwa ni India. Na hawakufika huko

usiku mmoja usiku kucha, na wakaanza kwenye usiku mmoja na kufika usiku uliofuata, walichukua yapata miaka miwili kufika kule. Hawakukijia Kitoto kichanga kwenye hori. Walimjia Mtoto mdogo, Mtoto mdogo. Ndipo Herode akawaua watoto kuanzia miaka miwili. Mnaona, kujua kwamba hakikuwa ni kitoto kichanga kimelazwa horini, angeviua tu vitoto vichanga. Lakini aliwaua watoto wadogo, ili awe na hakika kumpata Huyo, popote kuanzia umri wa miaka miwili kurudi chini. Aliweka wakati huo kwa sababu akijua hakutaka kuwaua wengi kupita kiasi, wote hao, alininii tu. . . maana walikuwa zaidi ni kama watumwa kwake. Alitaka kupata. . . kuwa na hakika kumpata Yeye, kwa hiyo akasema, "Huyo Mtoto atakuwa na yapata umri wa miaka miwili. Kwa hiyo, kila kitu kuanzia miaka miwili kurudi chini, kiuliwe." Mnaona?

Na hilo limefanya kutimia yale ambayo nabii alisema, kwamba, "Katika—katika Rama kutasikika ma—mayowe au kilio, maombolezo; Raheli akiwalilia watoto wake, kwa kuwa hawako."

49 Sasa, hivi ulitambua kwamba hawa mamajusi, watu mashuhuri, walikuwa huko Babeli ndipo wakaona Nyota Yake, tukasema, "Tumeiona Nyota Yake mashariki nasi tumekuja kumsujudia." Wakaja kutoka mashariki, ambapo waliiona hiyo Nyota, wakienda magharibi. Kwa sababu India iko magharibi, magharibi ya kaskazini mwa Bab-. . . mwa—mwa Palestina. Ndipo wakaja moja kwa moja kupitia Mto Tigris na kuvuka mahali tambarare wakiendelea, wakateremka kuingia Bethlehemu mahali walipompata M—M—Mtoto huyo. Basi kumbuka Yusufu na hao wengine hawakutoka huko; walienda moja kwa moja huko Nazareti na kumlea Mtoto huyo, pale pale.

50 Sasa, tunaona hapa kwamba waliwasilisha. . . Watu hawa, wakiwa ni wanajimu na kuangalia nyota, na kuona nuru hizi za ajabu za kimbinguni zikionekana huko juu, kwamba kulikuwa na jambo fulani likiendelea; hata walijua kwamba huyo ni Masihi, M—Mtawala wa mbingu na nchi, alikuwa azaliwe. Basi wakaja, wakijua kwamba Mungu angetiwa ndani, kuwekwa ndani ya nyumba ya—ya binadamu; maana kuwaonyesha ushuhuda wao. . . Unajua, unajua, maisha yako hunena kwa sauti kubwa zaidi kuliko maneno yako, mpaka haijalishi unasema nini, watu wanajua kile ulicho kwa—kwa kile ulicho.

51 Basi waangalie watu hawa, hawa Mamajusi, walimletea Yeye. . . Angalia tunu walizomletea Yeye, zilitambulisha kile walichofikiri Yeye alikuwa. Walimletea dhahabu, uvumba, na manemane. Na sasa angalia kile mifano hii, ninayotaka kuwazungumzia juu yake sasa . . . ni kile mifano hii inamaanisha. Sasa, ninayo Maandiko fulani yaliyoandikwa hapa ambayo tutasoma katika dakika moja tu kuhusu hilo, Bwana akipenda.

Sasa: dhahabu, na uvumba, na manemane.

52 Sasa: dhahabu katika Biblia . . . jinsi ifaavyo inavyomfaa Kristo, kwa sababu dhahabu huzungumzia Uungu. *Dhahabu* ni "Uungu." Tutaifikia katika dakika moja. *Uvumba* huzungumzia "huduma." Na *manemane* ni "mauti." *Mungu, Uungu, katika huduma ili kufa.* Na hicho ndicho alichokuwa. Kitu chenyewe walicholeta kilitambulisha kile walichowazia Yeye alikuwa.

53 Nami nasema hilo kwetu leo hii, "Vitu tunavyomletea Yeye hutambulisha yale tunayowazia kumhusu Yeye." Mnaelewa ninachomaanisha? Mnaona? Kama wewe ni . . . Kama unaamini Hilo kwa moyo wako wote, kila Neno la hiyo, utatambulisha hilo kwa kutoa yote uliyo nayo kwa Hilo. Mnaona? Bali kama unaamini kuwa ni mahali pazuri pa kushirikiana na watu walio bora, karibu na kanisa na mambo kama hayo, karibu hayo ndiyo unayotoa (saa chache tu za kijamii pamoja na baadhi ya kusanyiko au kitu fulani). Lakini kama kweli u—unaamini Hilo kwa moyo wako wote, basi unatoa yote yaliyoko ndani yako kwa ajili Yake. Unaona? Na inakutambulisha, kwamba kweli unaamini Ujumbe, kwamba unauamini kuwa ni Kweli.

54 Watu wengi sana wanasema, "Ninaweza kuamini kiasi *hiki.* Ninaweza kuamini *hivi.*" Wanafunzi . . . Ninaamini wakati uliopita hapa, nilizungumza juu ya hilo: *Waaminio, Wanaojifanya Waaminio, Na Wasioamini.* Sivyo ilivyokuwa? Mimi . . . si nilizungumza juu ya hilo hapa? Unaona? Na kila mtu, angalia aina yao. Mnaona, itafikia mahali ambapo wanaweza kuchukua kiasi fulani chake, hawawezi kuchukua yaliyobaki.

55 Sasa, jinsi tunu hizi zilivyoafiki safari ya Kristo duniani, Mtoto aliyezaliwa hapa duniani. Na tunu hizi ambazo mamajusi walimletea, ziliafiki hasa agizo Lake kutoka kwa Mungu na safari Yake duniani.

56 Sasa, jambo la kwanza: Mungu. Huyu alikuwa ni Mungu, Yesu alikuwa ni Mungu katika umbo la binadamu. Hilo ni gumu kwa watu kumeza hilo, hata leo, kwamba "Yeye alikuwa Mungu." Na Yeye . . . Hicho ndicho alichokuwa. Hakuwa chochote pungufu ya Mungu. Alikuwa ni Mungu akidhihirishwa katika mwili. Alikuwa ni Muumba katika kiumbe Chake Mwenyewe. Sasa hilo . . . Alikuwa ni Muumba ndani ya kiumbe Chake, kwa kiumbe, kwa ajili ya kiumbe. Alikuwa ni Muumba ndani ya kiumbe Chake, kupitia kiumbe Chake, kwa ajili ya kiumbe Chake. Yote yanarudi moja kwa moja ndani ya Mungu, kitu chote. Hivi hamwoni? Utimilifu wa Mungu! Yeye alikuwa ni Muumba kiasi kwamba alikuwa Mungu. Na Yeye alikuwa ni Kiumbe duniani (Kiumbe cha wakati), ambalo linamaanisha kwamba Yeye lazima alikuwa na mwanzo, hivyo basi Yeye alijiumbia Mwenyewe mwili wa kuishi ndani. Mungu, Mwenyewe, alijiumbia Mwenyewe mwili. Mnaona? Kwamba kwa

kiumbe hiki, Yeye aweze kuokoa kiumbe kilichopotea ambacho Yeye alikuwa ameumba.

57 Hakuna kitu ambacho mwanadamu anaweza kuangamiza, hakuna kitu kimoja. Huwezi kufanya chochote kuangamiza kabisa kitu chochote. Unaweza kuchukua kipande cha karatasi na kukiteketeza, waweza kuteketeza jengo, huenda ukachoma mti; hukuuangamiza. Wewe. . . huo moto humo ndani, huo moto unaotokea, hizo tu ni kemikali zikipasuka. Zinarudi kwenye kile zilichokuwa hapo mwanzo. Hazijaangamizwa. Ukichoma kipande cha mbao (na ulimwengu, tuseme, kama tuliishi katika Umilele kama Mungu, na hizo kemikali kutoka kwa hiyo mbao na moto huo zilirudi kwenye mwanzo wake wa asili na ninii yake. . . katika chochote zilichokuwa, kuvunjika kwa atomu na kadhalika, u—ulimwengu, tuseme, ungesimama kwa mamilioni ya miaka), hizo zingerudi moja kwa moja tena na kuwa mti mwingine, kama tu ulivyokuwa hasa.

58 Huwezi kuangamiza chochote kwa sababu ni Neno Lililonenwa la Mungu. Amina! Loo, na hilo linanifanya kujisikia kubarikiwa, sasa. Unaona? Lile Mungu asemalo, Hilo husimama milele. Amina! Unaona, huwezi kuangamiza. Sisi ni sehemu ya dunia hii, na hatuwezi kuangamizwa kabisa. La, bwana. Dhambi (nafsi) itaangamizwa, tunatambua hilo. Lakini m—mwili tunaoishi ndani yake, hauwezi kuangamizwa. Unaona?

59 Sasa, hivyo basi, Mungu alijiumbia Mwenyewe mwili. Alikuwa ndiye Muumba, na akaumba kiumbe Chake Mwenyewe, kwamba kwa Kiumbe hiki aweze kuwaokoa wale waliopotea katika maumbile Yake (hiyo ni mimi na wewe, viumbe vya wakati).

60 Ne—Neno Lake lilionyesha hakika kwamba. . . Yeye na kazi Zake zilithibitisha kwamba Yeye hakuwa chochote pungufu ya Muumba. Alichukua kipande cha mkate akaumega, na akaendelea kuumega kipande hicho kimoja cha mkate, na kuwalisha watu elfu tano kutokana na hicho; na vikachukuliwa vikapu saba vimejaa vipande vilivyobakia, na kila mtu pale a—a—alishiba kwa mkate.

61 Alichukua samaki na kuvunja huyo samaki. Sasa tukitambua kwamba Yeye alimwumba huyo samaki hapo mwanzo. Aliuumba huo mkate hapo mwanzo. Bali alichukua samaki huyo na kumvunja samaki huyo. Samaki alikuwa hai, kisha akachemshwa ama—ama kukaangwa; na wakati wowote alipommega, chochote kile (aliyechemshwa ama kukaangwa), aliongezeka tena (dakika ile ile Yeye alipommega) samaki mwingine aliyechemshwa au kukaangwa. Hiyo si ni ajabu? Hiyo ilionyesha kwamba Yeye alikuwa si chochote pungufu ya Yehova. Halafu basi Yeye alikuwa ni Muumba aliyeweza kuchukua kiumbe Chake Mwenyewe, na kupitia kiumbe Chake, aonyeshe kuwa Yeye ni Nani. Haleluya! Hiyo ilithibitisha kuwa

Yeye alikuwa kile Yeye alichokuwa. Alikuwa Mungu. Kwa hiyo, dhahabu ilimfaa, katika toleo wakati wa kuzaliwa Kwake. Alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili.

62 Huenda nikaingiza ki-. . .Hakuna wageni miongoni mwetu usiku wa leo, nadhani, kwa hiyo. . .katika mkutano huu wa maombi. Lakini hebu niseme jambo. Je! Yesu, wakati alipokuwa hapa,. . .? Sasa, hili ni la kutafakari, si la. . .labda. . .kudadisi hasa. Angalieni, kwa kutafakari tu, Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya na kubwa kuliko hizi atafanya, kwa kuwa Mimi ninaenda kwa Baba Yangu." Hivi mlitambua hilo? Angalieni, sasa, huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu akimwahidi mwaminio, kwamba mambo makubwa kuliko aliyofanya Yeye, (katika siku hizi za mwisho) kwamba mwaminio angefanya mambo makubwa kuliko aliyofanya Yeye. Yohana Mtakatifu, mlango wa 14, kifungu cha 12. Je! hiyo ni kweli? Je! mnaamini Yesu alisema hivyo?

63 Tazama, wakati Yesu alipoumba mkate; Yeye alichukua kipande cha mkate, akaumba mkate ambao tayari ulikuwa ni mkate. Alipoumba samaki; Yeye alichukua samaki ambaye kwanza aliumbwa samaki, na kuleta samaki mwingine kutoka kwake. Je! hiyo ni kweli? Alichukua maji, ambayo kwa uwezekano yangefanyika divai, na akatengeneza divai kutoka kwayo. Hiyo ni kweli? Bali tumemwona miongoni mwetu, katika siku hizi za mwisho, akiumba vitu moja kwa moja, bila ya chochote kilichosimama hapo! Je! hiyo ni kweli? Kuumba kuchakulo mahali hakuna kuchakulo. Kweli! Loo, Yeye ni. . . anabaki Mungu. Yeye ni Mungu tu leo kama alivyokuwa wakati ule na alivyowahi kuwa, ama atakavyowahi kuwa. Angali ni Mungu, na kuipa mioyo changamoto kuamini hilo, "Mambo makubwa zaidi ya haya, nyinyi. . .pasipo na kitu cha kushikilia na kumega kutoka kwake. Nena, na itakuwa hivyo."

64 Tazama sasa, tunaona ya kwamba ninii Yake. . .Yeye alitambulisha. Kazi alizofanya Yeye zilitambulisha kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, zilionyesha kwamba ndivyo Yeye alivyokuwa. Kwa kuwa Yeye alisema, "Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi."

65 Na je! hivi Mkristo leo hii asingeweza kusema, "Kama sizifanyi kazi za Mwokozi wangu, msiniamini"? Mnaona?

66 "Kama Baba alivyonituma Mimi, ndivyo ninavyowatuma Mimi." Na kama ulizifanya kazi, kazi za uumbaji wa Baba aliyemtuma, basi ni uumbaji. . .Kristo (Muumba) anayetutuma, huzifanya kazi za Kristo Muumba. Unaona? "Kama Baba alivyonituma Mimi, ndivyo ninavyowatuma Mimi. Na kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, msiniamini."

67 Basi Mkristo leo hii hana budi kutimiza Maisha ambayo Kristo alitimiza ama tuna haki ya kusema, "Sivyo."

68 Angalia sasa, kazi Zake zilimwumba Yeye...ama zilimtambulisha Yeye kuwa ni Muumba. Kazi Zake alizofanya zilivisha taji ushuhuda wa maisha Yake, kwamba yeye alikuwa ni "Muumba"; hamna njia ya kuondokea hilo. Hivyo basi, walipotoa tunu ya dhahabu, walikuwa kabisa katika mapatano na Mungu pamoja na tunu yao. Walimpa Yeye dhahabu, iliyomtambulisha kama Mungu. Daima taji, taji ya dhahabu... kichwa cha dhahabu, cha Mfalme Nebkadreza. Yote, mnaona, hiyo...daima Uungu unawakilishwa na dhahabu.

69 Sasa: *uvumba*. Tunataka kupata haya upesi. *Uvumba* ni "toleo la huduma kwa Yehova." Sasa, kama unataka kuandika Maandiko haya, Mambo Ya Walawi 2:2, na Mambo Ya Walawi 16:6 hadi 15. Tunaona kwamba huo ndio utaratibu wa ukuhani, kutoa sadaka kwa Yehova. Wakati alipotoa sadaka, ilibidi itengenezwe na kuchanganywa na uvumba kwa ajili ya toleo la dhambi, walichukua vitu mbalimbali na kuvichanganya. Kwa ajili ya toleo la unga, kwa ajili ya toleo la kutikiswa, uvumba uliongezewa. Kwa sababu, lilikubalika kwa Yehova ikiwa lilitiwa upako na *uvumba*, ambao unamaanisha kwamba ni "huduma kwa Yehova, Mungu." Tena, sasa, tunaona Yeye ni Mungu. Basi walimletea uvumba, ulikuwa ni mfano kwamba Yeye alikuwa ni huduma kwa Yehova. Yesu ni Mtumishi wa Yehova.

70 Sasa, katika Mathayo Mtakatifu 12:15 hadi 21, tunaona kwamba Yeye alikuwa ni Mtumishi wa Yehova, "Tazama Mtumishi wangu, ambaye ninapendezwa Naye" (na Yeye alikuwa) "na ninaweka nguvu Zangu juu Yake." Kwa hiyo maisha Yake yalitiwa upako na uvumba, kwa huduma ya Yehova. Ni tunu ya jinsi gani hawa mamajusi waliyotoa! Mnaona, kilikuwa ni kitu fulani cha...tu—tunu waliyoitoa, kilikuwa ni kitu fulani cha kumtambulisha Yesu kama Mtumishi wa Yehova.

71 Sasa laiti tungaliweza tu kufanya hivyo, kuyatambulisha maisha yetu. Mnaona, maisha yetu yatambulishwe kama mtumishi wa Yehova. Hiyo ndiyo iliyokuwa kazi ya uvumba, iliyomfanya Yeye Yehova Mtumishi.

72 Sasa, *manemane*, m-a-n-e-m-a-n-e, ilikuwa "upako wa mauti." Tunaona katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 19, kifungu cha 39, kwamba wakienda kwenye i—ibada ya mazishi ya Yesu, wakati Mariamu na wale wengine walienda, walibeba hii manemane kumpaka nayo; kwa sababu Yeye lazima awe ni Mtumishi wa mauti kwa Yehova. Mnaona? Mtu fulani ilibidi afe. Hiyo ilikuwa ni huduma ambayo ilibidi itekelezwe kwa Mungu, na hakuna mtu aliyestahili kuifanya ila Mungu Mwenyewe. Kwa hiyo, kuleta manemane—manemane, ikionyesha kwamba pamoja na Uungu, na pamoja na huduma, kwamba Yeye pia alipakwa na manemane; kwamba Uungu huu ilibidi uwekwe mautini ili kumwokoa asiye mkamilifu. Loo, ni jambo kuu jinsi gani!

73 Maumbile yote yalikuwa yamepotea. Ndio kwanza tulipitie katika Mihuri Saba. Mnaona, maumbile yote yalikuwa yamepotea, kila kitu kilikuwa kimekwisha. Yote yalikuwa mkononi mwa Shetani. Aliurithi na angali anaumiliki. Hakika anaumiliki. Hiyo ndiyo sababu tunapigana na kuwa na matatizo haya yote. Anatawala kila ufalme; Shetani anatawala. Kila serikali, kila mfalme, kila ufalme, unatawaliwa na Shetani. Ulimwengu wote unatawaliwa na kuongozwa na Shetani. Hiyo ndiyo sababu tuna shida tulizo nazo. Mwanafunzi yeyote wa Biblia, ama chochote, anaweza kukuambia kwamba Shetani . . . Vema, Biblia Yenyewe inasema alifanya hivyo, mnaona, kwamba anatawala ulimwengu. Bali Kristo atakuwa Mrithi wake, kwa sasa Yeye ni Mkombozi wetu. Na Yeye alikuja kukomboa maumbile yote, na hakuna chochote kingaliweza kufanya hivyo ila Mungu Mwenyewe.

74 Hiyo ndiyo sababu kwamba Mungu hafanyi chochote nje ya mwanadamu. Yeye daima hufanya kazi kupitia mwanadamu kwa sababu ilimbidi Yeye kumtumia mwanadamu. Mwanadamu ndicho kitu kilichomlazimu kutumia ili kuonyesha sifa Yake ya kuwa Mwokozi. Ilimbidi kumwumba katika sura Yake, kumfanya kitu kinachofanana na Yeye, na kumweka katika hiari ya kujiamulia na kumwacha atende kwa njia yoyote aliyotaka. Angeweza kujiamulia. Na Yeye alijua kwamba mwanadamu, kwa kumpa chaguo hili, angeanguka. Kwa hiyo kwa kuwa ilimbibi kufanya hivyo, Yeye anageuka na kumfanya mwanadamu mwenzi Wake, na hafanyi chochote isipokuwa Yeye afanye kupitia mwanadamu!

75 Kazi yote ya ukombozi ilikuja kupitia mwanadamu! Haleluya! Kifo kilikuja kupitia mwanadamu wa kwanza, Uzima ukaja kupitia Adamu wa pili. Unaona? Haya basi, Yeye hafanyi chochote kwa sababu ilimbidi Yeye kutumia mwanadamu kwa hicho, ndipo Yeye anamtumia mwanadamu kukomboa tena. Kwa hiyo Mungu alifanyika Yehova, ama, Yehova ali-. . . Yeye ni Mungu, na alifanyika M—Mtoto. Alikuja katika umbo la dhambi, ili Yeye aweze kumkomboa mwenye dhambi. Unaona, hicho hapo kitu chote.

76 Sasa, angalia kile . . . jinsi tunu hizo zilivyoafikia vizuri ndani ya Yesu Kristo; unaona, dhahabu, ikizungumzia Uungu Wake. Sasa, hawakuwa makafiri. Walivuviwa na Mungu. Hawakuwa wakidhania kitu fulani. Hiyo inathibitisha papo hapo, hata Mamajusi, kwamba waliona cha Kimbinguni. Kwa sababu zawadi yao wenyewe, waliyoitoa, ilitambulisha na kunena mema juu ya ushuhuda wao kwamba waliona Nuru ya Kimbinguni. Kwa sababu nini? Inanena kikamilifu. Walileta *dhahabu*, "Uungu." Walileta *uvumba*, "huduma." Pia walileta *manemane*, kwa ajili ya "kifo" Chake, wakati alipokuwa ni Mtoto mchanga, amina, ikionyesha kwamba Mungu atatiwa

mautini katika mwili, amina, kusudi imkomboe mwanadamu aliyeanguka. Watu wanawezaje kulikataa hilo?

77 Unapotambua: Tunafanya nini hapa? Tulitoka wapi? Ama ni nini sababu yetu ya kuwa hapa? Hatukuwekwa hapa tu kibahati, tuliwekwa hapa kwa kusudi na hatuna budi kutumikia kusudi hilo. Lakini bado tumerudi katika msingi wa hiari ya kujiamulia ambapo tunaweza kutumikia Hilo ama kulikataa Hilo, kama vile tu Adamu alivyofanya pale mwanzo.

78 Ninawaangalia, hawa wasichana wadogo hapa, Ndugu... Ni nini...? Ninaamini ni maskini mama huyo aliyepiga piano, nami ni—nilikuwa nikiwasikia walipokuwa wakiimba. Tulikuwa tukiongea juu yao, njiani tukipanda kuja hapa. Hiyo hapo familia ndogo iliyotoa maisha yao yote na kila kitu kwa Kristo. Iangalie familia hiyo, jinsi ilivyo na utaratibu. Waangalie wasichana hao wadogo. Walikuwa wamesimama hapa juu, m—mfano wa ujana uke, wa utineja. Na haijalishi...

79 Majuma machache yaliyopita niliteremka chini katika kama...Sijui jina la mahali hapo huko chini, katika New York sasa, ambapo wanayo majengo tu ya mji ya watovu wa maadili. Sasa, hao wasichana huko chini wakiwa—wakiwa wamevaa legotadi na—na hakuna chochote kingine ila moja ya hizo maskini bikini ndogo, wanavyoiita, juu ya hiyo. Na, loo, ni mkusa-...Wanafanya chochote kilichoko niani mwao, haijalishi ni nini, hiyo ndiyo sababu—sababu ni wapinga maadili. Wanaweza kufanya tu chochote. Wakitaka kulala chini, wasiamke, wanalala tu chini na hawaamki. Wakitaka kwenda, kufanya jambo fulani, wanafanya hivyo; kama hawataki, hawafanyi. Ni kwamba, nia yao inasafiri tu! Nayo nia isiyoongoka hufikia nini? Huna haki ya kufanya hivyo, maana wewe si mali yako; umenunuliwa na Mungu, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliyefanyika mwili. Lakini, unaona, lundo la dhambi!

80 Halafu unaona maskini wasichana, wachanga namna hiyo wakijitokeza; kwa nini, kwangu mimi, ni nuru kwenye wakati wa giza. Ni nuru iliyogawanyika, ya mjeledi wa Mungu uliopindapinda, katika anga kuonyesha kwamba kunaweza kuwa na Nuru! Kunaweza kuwa na haki katikati ya dhambi!

81 Mariamu, mama wa Yesu, katika mji wa Nazareti, mji duni kuliko yote uliokuwapo nchini, bali kutoka pale Mungu alichagua mama mdogo kumzaa Mwana Wake; kiangulio, tumbo la uzazi ambalo ilibidi...ilibidi Mtoto azaliwe kwalo. Alimchukua mtu kama huyo kufanya hivyo. Mungu hufanya kazi kupitia wanadamu kuwakomboa wanadamu. Anaweza kukuchukua, afanye kazi kupitia wewe ili kukomboa wanadamu, iwapo utasalimisha kabisa kila kitu ulicho.

82 Kama wewe ni msichana, salimisha maadili yako. Wewe ni kijana mwanamume, salimisha maadili yako, salimisha nia yako, salimisha mawazo yako, salimisha moyo wako, salimisha

nafsi yako, salimisha yote uliyo! Na umwache Kristo afanye kazi kupitia hayo. Ni jambo tukufu jinsi gani! Unayo mito ya kuvuka, unayo ma—madaraja ya kupitia, unavyo—unavyo viunga vyenye miiba, unavyo vichaka, unayo misitu, una mahali pa giza, unavyo vilima virefu, una mahali pa kupanda juu. Unafanya nini? Siku moja itakubidi kusimama na kutazama nyuma, uone mahali ulipotoka, nawe utahukumiwa na ile njia uliyochukua. Weka yote uliyo na—nayo, nia yako na mawazo yako, juu ya ile Nyota ya Kaskazini (kitovu cha Mungu) na usisogee kutoka Kwake. Dumu moja kwa moja na Hiyo. Itakuleta moja kwa moja kama ilivyowaleta wale Mamajusi, moja kwa moja hadi kwa Kristo.

83 Vema, wakampaka na manemane. Tunaona sasa, katika Yohana 12:1 na 7, hiyo hasa ndiyo Yeye aliyofanya. Alikuwa ni Mtumishi mkamilifu wa Mungu, na kumpaka na karama Zake zote za Kiungu. Alipakwa na karama zote za Mungu kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu. Alikuwa Mungu. Unaona, *wao* walimletea zawadi.

84 Sasa, tutakuwa. . .Natamani. . .Watu hapa daima, wengi wao, mnajua, hukutumia kitu. Sasa, ikirudi katika kuwatumia pia, nisingeweza kufanya hivyo. Mnaona? Ni ulimwenguni kote. Nisingeweza kabisa kufanya hivyo. Nami ninafurahia kidogo. . . vitu vidogo, na mambo ambayo watu hutenda ili kujieleza na shukrani zao na kadhalika.

85 Sasa, hili ndilo hao matajiri walifanya. Watu hawa ni Mamajusi, walinunua dhahabu, dhahabu safi. Walileta uvumba, bora kuliko wote walioweza kupata. Walileta manemane, bora zaidi waliyoweza kupata.

86 Tunatambua hapa, katika Yohana Mtakatifu 12, tunaona kwamba mwanamke huyu. . .kama tungalikuwa na wakati kuisoma, lakini sitaki kuwaweka muda mrefu sana, mnaona, maana ninajua kesho ni Jumatatu, na nyinyi. . .baadhi yenu inawabidi kufanya kazi. Angalia, walileta. . .Mwa—mwanamke huyu alileta hii manemane, hicho kitu chenye bei ghali kilichotiwa upako, kuondolea mbali harufu mbaya ya kifo. Basi akapasua kibweta cha marhamu na kuimimina juu ya kichwa cha Yesu. Ndipo Yuda akasema, "Mbona, hii ilipaswa kupewa maskini." (Kasema, "Si kwamba aliwajali maskini, bali alikuwa ni mwizi kwa kuanzia, alibeba pesa.") Na kasema, "Hii ilipaswa kuuzwa, badala yake umeiweka. . . "

87 Naye Yesu akasema, "Achana naye! Kwa kuwa alifanya hili. . . " Alimpaka Yeye mafuta, kwenda kwa mazishi Yake. Mnaona? Mwanamke huyu, akiwa na shukrani sana kwamba dhambi zake zilisamehewa mpaka akatumia pesa zake zote alizokuwa nazo, na kuchukua kibweta cha marhamu na kukipasua na kumimina mafuta na kukitia chumba manukato kwa harufu nzuri ya hii manemane, aliyokuwa amempaka nayo

kwa ajili ya kifo Chake. Sasa, mnaona, alifanya huduma hiyo bila kujua alichokuwa anafanya, bali alikuwa na shukrani tele kwa Mungu.

88 Basi kama una shukrani sana kwa ajili ya Krismasi, si kusema, "Ni—niliwapa kina Jones zawadi; nao wakanipa moja pia, nitaona nilicho nacho asubuhi." Mbona usifungue moyo wako na uone kilichoko humo, tafuta kujua kile ulicho nacho *hapa* ndani. Na ukubali . . . tukiupata ukiwa mtupu, ukiwa tu na kanuni mbaya za imani na—na—na mahangaiko ya ulimwengu, kwa nini usimwombe Kristo aujaze usiku wa leo? Usiku wa leo, kusudi uweze kupata maana halisi ya Krismasi. Ni—ni Kristo ndani yako; Mungu, akikaa katika moyo wa mwanadamu. Hiyo ndiyo Krismasi halisi inayomaanisha.

89 Lakini, unaona, leo hii tunakuwa wasiojali sana. Ni ibilisi akitupitisha pale, (kuna vijiti vya peremende vilivyopakwa rangi, na ninii—na kulungu wa nchi za baridi na—na mtu mwenye masharafa, na kupaa kupitia hewani kama ndege, na kuzuru ulimwengu mzima na kila nyumba akiwa na kifurushi kidogo cha wanasesere mgongoni mwake, na kumtembelea kila mtoto) na ni—ni uongo mtupu! Ni, uongo tu, kabisa. Mnaona? Sasa, mnaona? Lakini ni kwa nini? Ibilisi alifanya hivyo kusudi aweze kupotosha nia za watu.

90 Ulimwengu wa biashara uliingia katika hiyo na wao . . . Mbona, wanapata ya kutosha kupitia wakati wa Krismasi mpaka karibu, wanaweza kupumzika mwaka mzima. Nilizungumza na mfanyabiashara hivi majuzi, akasema, "Nipe majuma haya mawili, na kama haikunibidi kuwaweka watu wangu hapa," kasema, "Ningengojea mpaka Krismasi ijayo; ningeweza kwenda kuvua samaki, chochote nitakacho kufanya, hadi Krismasi ijayo." Akasema, "Lakini ninawatunza hao wavulana." Kasema, "Ninawaweka tu hapa vya kutosha kuifungua biashara yangu na inanipa—inanipa riziki na kadhalika." Kasema, "Sipati chochote mpaka—mpaka ifike wakati wa Krismasi." Mnaona, imekuwa ni kitu kikubwa cha biashara wakati inapaswa kuwa ni ibada; kuabudu.

91 Sasa, Mungu, alimpaka sana Yesu na utimilifu Wake Mwenyewe hata ninii . . . Yeye alikuwa ni Karama ya Mungu kwa ulimwengu. Hata mamajusi wametambulishwa wazi, kwamba wanatoa tunu yao Kwake; ilionyesha kwamba moyoni mwao walijua kwamba Yeye alikuwa ni nani, na kile Yeye alichokuwa anaenda kuwafanyia. Kwa hiyo (si ajabu) jambo la kwanza walilofanya, waliinama chini, kikamilifu kabisa, na kumsujudia. Hata kabla hawajalielewa, waliinama chini na kumsujudia na kisha wakawasilisha tunu zao. Hiyo ndiyo njia ya kuwa na Krismasi halisi: kumsujudia Yeye, halafu uwasilishe tunu yako; ukiutoa mwili wako kama dhabihu iliyo hai, takatifu na inayokubalika kwa Mungu.

92 Lakini mnajua nini, baada ya mamajusi kufanya hivyo? Baba na mama wa Kristo…baba mlezi (bila shaka) na pia mama, kwa sababu Mungu alikuwa ndiye baba Yake na mama pia. Lakini tunapata kwamba walipokea tunu hizi kutoka kwa hawa mamajusi. Si ajabu waliitwa wenye hekima. Walikuwa wenye hekima. Walikuwa ninii kwelikweli…walikuwa na busara. Laiti watu leo hii wangekuwa na hekima hivyo, wenye hekima tu hivyo! Inahitaji mtu mwenye busara kumjia Kristo. Mtu anayegeuka kuondoka Kwake ni mtu asiye na hekima. Bali inahitaji mtu mwenye hekima, kumjia Kristo.

93 Sasa angalia! Basi baada ya hapo hao mamajusi wakimtambua kile ambacho Yeye angekuwa, na tunaona kupitia Maandiko hicho ndicho hasa alichokuwa: Uungu katika huduma kwa ajili ya kifo. Kwa nini? Uungu katika huduma kwa Mungu kwa ajili ya mauti. Yesu alikuwa ni Uungu katika huduma kwa ajili ya mauti, kuukomboa ulimwengu. Lakini ulimwengu uliufanyia nini Huo? Waliukataa Huo. Waliukataa Huo. Kwa nini? Baadhi yao, sehemu kubwa yao, walifanya hivyo kwa sababu hii: kwa sababu Yeye alikufa! Wakasema, "Asingeweza kuwa Mungu na afe." Huyo Mtu (mwili) hakuwa Mungu, bali Mungu alikuwa ndani ya mwili. Mwili huu hauna budi kuangamia. Kristo mwenyewe aliye ndani yako ndiye kitu cha pekee kinachoweza kukufufua. Huo ni Uungu, Mungu ndani yako.

94 Sasa, tazama! Sasa, sawa na ilivyo sasa, wanamkataa Mungu aliyetambulishwa. Mnalipata? Hakika wataweka jina lao kwenye kitabu cha kanisa na kusema, "Nitajaribu kuishi kwa kanuni hii ya imani." Wataapa kwa hili. Bali inapofikia kuukubali Uungu, na kuonyesha aina ile ile ya tunu kama walivyoonyesha…kwamba umetambulishwa na tunu yako, kwamba unatoa utu wako wote Kwake, kwa Mungu aliyetambulishwa. Basi unajitambulisha mwenyewe na Mungu, kwa kutoa yote uliyo, kile ulicho, kwa Mungu Mwenyewe.

95 Sasa, Kristo katika siku hii, ambayo tunaishi sasa, angali ni Mu-…akijitambulisha Mwenyewe: Mungu, miongoni mwa watu. Angali ni Mungu, kwa sababu Yeye ni Neno. Ndipo tukiliona Neno likiishi Lenyewe, basi tunajua kwamba mwanadamu hawezi kufanya hayo. Ni Mungu, Neno likidhihirishwa na mwanadamu. Naye Yesu alisema Mwenyewe, "Mwana hawezi kutenda lolote Mwenyewe. Siwezi kufanya lolote, mimi ni Mwanadamu," Yesu alisema. "Ila Baba Yangu aishiye ndani Yangu, Yeye hunionyesha mambo yote ambayo Mwenyewe anatenda." Amina! Haya basi! Ni kitu gani? Mungu akitambulishwa katika mwanadamu. Sasa, jambo lile lile lipo leo hii; kwamba Mungu, Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii, linaweza kujitambulisha Lenyewe ndani yako. Amina! Basi toa yote uliyo nayo Kwake. Onyesha kwamba unaamini Hilo. Lipe Uungu: amini Hilo, huduma, na uwe tayari kujifia mwenyewe

na mawazo yako mwenyewe. Lakini leo hii Hilo limekataliwa kama lilivyokuwa wakati ule.

96 Angalia, Mungu aliwaongoza Mamajusi pamoja na tunu hizo. Kwa yapata miaka miwili, waliifuata ile Nyota. Mnaona? Na hiyo inaonyesha kwamba Hiyo isingeweza kuwa ni moja ya mambo ya kawaida yaliyotendeka. Mnaona? Kwa sababu kama nyota, zikivuka mizingo yao, zingevuka, ingeonyesha kulikuwa na jambo tofauti. Kwa sababu. . .isipokuwa hao Mamajusi waliiona Hiyo, muda mrefu kabla ya hayo kutendeka, na kujua iliwabidi kuivuka njia hiyo; unaona, katika njia walizokuwa wakijia. Nao wakavuka tu huko Bethlehemu wakati huo, wakaanzia huko juu, hapo kabla, wakijua kwamba viumbe hivi vya kimbinguni vilikuwa vikienda njia hiyo.

97 Sasa, Mungu aliwaongoza Mamajusi kwa sababu walikuwa na tunu zifaazo. Mungu aliwaongoza watu hawa wenye hekima kwa sababu walikuwa na tunu iliyotambulishwa vizuri kumtambulisha Mwana Wake. Looooo, jamani! Mnalipata? Watu wenye hekima leo hii, wanainuka katika Jina la Bwana, sio na kitu fulani cha kubuni, bali na tunu ambayo Mungu aliahidi kwa ajili ya siku hii, naye Mungu atakuongoza ili kutambulisha kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Haya basi: watu wenye hekima!

98 Mungu aliziongoza zawadi hizo kwa sababu zilikuwa ni zawadi za kumtambulisha Yeye. Watu wenye hekima, leo hii, ambao wanaweza kutazama mbali na ukanisa na mambo yote ya ulimwenguni, walitazame Neno Liishilo la Mungu! Basi Mungu atamtambulisha Mwana Wake kwa Neno Lake, kwa sababu Hilo ndilo alilo Yeye. "Mimi na Baba Yangu tu kitu kimoja." Na, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa katikati yetu." Basi Neno lile lile leo hii, Yeye ni yule yule jana, leo na hata milele. Na mtu mwenye hekima hufuata Hilo, kwa sababu Hilo ndilo Mungu hutunza kujitambulisha Mwenyewe kwa Hilo. Amina! Karama! Karama halisi iliyotambulishwa ya Mungu, Mungu huileta kupitia kila kitu namna hiyo, kujitambulisha Mwenyewe kwalo.

99 Na hivyo ndivyo Kristo alivyotambulishwa: na dhahabu, manemane, na uvumba, kwa watu hao wakionyesha kimbele na kuonyesha katika mfano kile maisha Yake yaliyopaswa kuwa. Mnaona? Mungu akidhihirishwa kwa ajili ya huduma, kufa ili Yeye aweze kulikomboa taifa, kwa sababu Yeye alipaswa "kuwaokoa watu Wake kutoka kwa dhambi zao." Si kuokoa ulimwengu, kuokoa watu Wake kutoka kwa dhambi *zao*. Biblia ilisema hapa, "Kwa kuwa katika—katika Jina Lake Mataifa watatumainia." Mnaona? Mataifa watatumainia Jina Lake. Amina! Kwa maneno mengine, Bibi-arusi, *walioitwa watoke* wa Mataifa, watakuwa wakitumainia Jina la Yesu Kristo, "Katika Jina Lake Mataifa watatumainia." Sasa, Mungu aliwaongoza,

kwa kuwa walikuwa . . . zawadi walizokuwa wakitoa, zilifaa kwa wakati.

100 Tazama! Kama nilivyosema, Mungu anayo . . . Yeye—Yeye aliligawa Neno Lake pale mwanzoni, katika Mwanzo. Ninaweza kuchukua Mwanzo na kuwaonyesha kila wakati kwenye Biblia, hadi kufikia wakati huu hapa. Madhehebu yote na vitu tulivyo navyo leo hii, ninaweza kuwaonyesha mahali hasa vilipokuwa katika Mwanzo. Mnaona?

101 Mungu alitoa Neno Lake kiasi fulani *hapa*, kiasi fulani *hapa*, kiasi fulani *hapa*, kwa kila wakati. Ndipo basi akamtuma nabii chini, akamtia upako kulifanya Neno hilo litimie, nalo linaunga mkono lile lingine lililopaswa kuja. Mnaona, kama vile Masihi, daima aliunga mkono. Kila nabii katika maisha yake mwenyewe, utu wake wenyewe, Neno lililotolewa kwa ajili ya siku hiyo, alikuja na kutimiza hilo Neno lililoandikwa na kutabiri kile lile lingine lilikuwa linaenda kuwa. Basi kila mmoja wao alinena kumhusu Yeye (amina) maana Yeye alikuwa ndiye utimilifu, Yeye alikuwa ndiye Kichwa cha manabii, Yeye alikuwa ni Neno la Mungu, Yeye alikuwa ndiye manabii. Amina! Huyo hapo. Angalia! Ni ajabu jinsi gani kile Yeye alichokuwa: kila mmoja wa hao manabii.

102 Ndipo wakati Yeye alipokuja, alikuwa ndiye utimilifu wa manabii wote, ukidhihirishwa; maana wao walikuwa ni Neno la Bwana, na Yeye akasema Mwenyewe, "Kama mnawaita miungu, wale waliojiliwa na Neno la Mungu, mnawezaje kunihukumu Mimi ninaposema 'Mimi ni Mwana wa Mungu'?" Mnaona, hata wale katika wakati huo walitambulishwa kama miungu, Mungu aliwaita, Mwenyewe, "miungu." Walikuwa ni nini? Walikuwa ni madhihirisho ya Neno Lake. Na hapa Yeye alikuwapo, utimilifu wa Neno, Mungu katika mwili, Mungu akidhihirishwa katika mwili.

103 Tazameni! Kwa zawadi hizi, ambazo watu hawa walileta, wasingeweza kuleta hizo kwa nabii. Isingekuwa sawa. Mnaona? Zawadi hizo zisingemwendea Eliya, zisingemwendea Musa, ilibidi zimjie Yeye. Na kwa kuwa zawadi hizo hasa zilikusudiwa siku hiyo, na zilikuwa zitambulishe kuwa Yeye ni Nani kwa zawadi hizi, basi hapa akaja Mungu moja kwa moja na kumlinda Yeye. Na kuwadumisha, miaka miwili huko chini, mpaka wakaipata ile Nuru Kamilifu. Jinsi inavyoafiki!

104 Jambo lile lile leo hii. Tunao watu ambao ni watiifu kabisa, watu wema, watu halisi. Bali, unaona, katika hilo, kunaenda kuwa na jambo litakalotokea, ambalo Mungu ametenda daima, kuitambulisha siku hii. Hii ndiyo siku ambayo mambo haya yamenenwa ili kufanyika. Hakutakuwa na wengi, ni wachache tu, wachache sana watakaookolewa. Biblia ilisema hivyo. Kutakuwa na wachache tu.

105 Yesu alisema Mwenyewe, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa." Watu wanane, kutoka kwa ki—kizazi kilichofananishwa na hiki. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Ilikuwa ni kitu gani? Watu mashuhuri, waliostaarabika, wafanyakazi mashuhuri, wajenzi mashuhuri, kila kitu mashuhuri kama walivyokuwa navyo. Wakafanya ustaarabu huu kama ulivyokuwa, mambo makuu waliyokuwa nayo. "Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu." Mnaona? Basi Mungu alimfanya Nuhu kulitambulisha Neno Lake lililoahidiwa. Lilifaa sana. Safina ilifaa Neno la Mungu alilonena, kwamba Yeye angemwangamiza mwanadamu. Lakini aliokoa kile angeweza.

106 Sasa, hawa mamajusi, wakileta zawadi zao, zilitambulisha. Zawadi zao zilitambulisha kile Hicho kilichokuwa, na hiyo ndiyo sababu ya Mungu kuzilinda zawadi hizo kupitia kila hatua waliyopitia. Alilinda Hicho mpaka wakafika na zawadi hizo, kwa sababu zilifaa kwa wakati huo. Je! kanisa langu linaelewa hilo? Hilo ndilo linaloendelea sasa! Natumai haipiti juu ya kichwa chako. Inanibidi kulinena katika methali, karibu, mnaona. Lakini je! mnaona? Ni mambo yanayotendeka yanafaa kwa ajili ya siku hii, Laodikia. Ni wakati ufaao, hiyo ndiyo sababu Mungu amelinda Hilo. Mnaona, akalileta Hilo kote moja kwa moja kujitambulisha Mwenyewe. Tunu, japo ziligharimu mauti, ziliweka jiwe la kujikwaa njiani mwao. Ni wakati ufaao, hiyo ni kweli, unaofaa kwa siku hii. Hiyo ndiyo sababu Mungu amelilinda Hilo, jinsi Yeye alivyofanya. Atalilinda Hilo, mpaka kusudi Lake litimizwe.

107 Loo, nilisoma hadithi fulani, nimeikumbuka si muda mrefu uliopita, ya kitu cha namna hiyo. Kulikuwa ni mji mashuhuri, hapa katika taifa hili, na. . .New York. Na ilikuwa kwenye mkesha wa Krismasi. Basi kulikuwa na familia maskini. Maskini baba mkongwe, alikuwa na TB, na alikuwa. . .na mke wake alikuwa na TB. Walikuwa ni wasio nacho. Na yeye—yeye kwa namna fulani. . .Alikuwa amedhoofika na kwa hiyo hakuna mtu angalimwajiri. Hakuwa na elimu, na yeye—yeye. . .watu hawakumpenda.

108 Alikuwa tu ni mtu aliyetengwa na jamii, akawa msokwao. Ninii tu. . .Mnajua msokwao ni nini, unaenda tu na—na kuchukua kitu, na kukichuuza na kupata kile uwezacho; ile faida ndogo wanayopata kwa hicho, wanajaribu kuishi kwayo. Ninii tu. . .kama mchuuzi au kitu kingine, mtaani; anaenda na kununua pini na sindano na kastabini, na chochote wawezacho. Na—na kuzichukua, na—na labda kununua kifurushi kimoja kwa senti moja, na kuziuza ndururu; na kupata senti nne kwa kifurushi, na labda katika mwendo wa siku moja. Unasema, "Hiyo ni—hiyo ni faida kubwa." Lakini hebu wazia tu, yote

ambayo angeuza kwa siku. Labda apate senti ishirini, thelathini kwa siku, naye alikuwa na familia.

109 Na ma—maskini mke, akiwa dhaifu, a—alifariki.

110 Na ulikuwa unakaribia wakati wa Krismasi. Basi msichana huyo mdogo, alikuwa amepatwa. . . kutokana na utapiamlo, kutokuwa na chakula kifaacho na kadhalika; akashikwa na TB, pia. Naye alikuwa ni jamaa mdogo, na yapata umri wa miaka minane, tisa, kumi. Naye hakuwa amewahi kuwa na mwanasesere kwa ajili ya Krismasi. Na huyo ndiye alikuwa anataka kama zawadi, alikuwa ni mwanasesere.

111 Naye baba, akiwa hawezi kumpa matibabu na kadhalika, alikuwa. . . a—alimwona maskini msichana huyo alikuwa anaenda upesi, basi alijaribu awezavyo ku—ku—ku—kuweka pamoja fedha za kutosha kumnunulia mwanasesere kwa ajili ya Krismasi; laiti angaliweza tu kupata fedha za kutosha kumnunulia maskini mwanasesere! Na kwa hiyo wakati wa Krismasi ulikuwa unakaribia, hali mbaya ya hewa ikaingia, maskini msichana huyo akashikwa na namna fulani ya nimonia, na—na akafa, majuma machache tu kabla ya Krismasi. Naye baba, bila shaka, akiwa amevunjika moyo, alienda kwenye mkebe wake mdogo na kutoa pesa. Ndipo akawazia kuhusu maskini msichana wake, na yeye alitaka m—mwanasesere kama wasichana wadogo. Mnaona, ni maskini mama akija.

112 Unatambua jinsi msichana mdogo, yeye anaendea mwanasesere, kwa sababu yeye. . . hayo ni maumbile yake, yeye ni—yeye anakuja kuwa mama. Atakuwa mama siku moja akiwa hai na kila kitu. Unajua, maumbile yake. Hiyo ndiyo sababu msichana mdogo hupenda maskini mwanasesere, anataka kumtunza; maana hata hivyo, yeye—yeye ni nanii mdogo, kwa uwezekano, ma—ma—mama mdogo.

113 Basi yeye alitaka maskini mwanasesere, na hakuwa amewahi kuwa na mmoja. Naye Baba alikuwa ameweka akiba kila alichoweza ku—kumnunulia mwanasesere. Na, kwa hiyo, akafariki.

114 Basi kidogo baba alikuwa na kupotea kwa akili. Mke wake alikuwa amechukuliwa, msichana wake mdogo, na akili yake ikafikia mahali hata yeye—yeye. . . bado ange—angeenda kulala kila usiku na kuongea na huyu msichana mdogo, ingawa alikuwa. . . alikuwa amezikwa. Lakini alidhania alikuwa—alikuwa anaongea naye, na kumwambia, "Sasa, Mpenzi, haitakuwa muda mrefu, na Baba anaenda kukununulia huyu mwanasesere kwa ajili ya Krismasi. Na—na Baba amekuahidi mwanasesere, nami ni—ni—ninaenda kumnunua."

115 Hatimaye, Krismasi ikawadia. Na, bila shaka, mnajua jinsi ilivyo. Matajiri walikuwa na ka—karamu zao kubwa; na—na mishumaa ikiwaka, na misa kubwa kubwa makanisani, na kuzungumza kuhusu Yesu na—na kadhalika (makanisa

yalikuwa), na kupitia kila namna ya taratibu za misa, na kuimba, na nyimbo za Krismasi na kila kitu. Hawakujua kile kilichokuwa kikiendelea huko nyuma kichochoroni, nyuma ya haya yote.

116 Maskini jamaa huyu huko nyuma, akarukwa na akili. Alitaka sana msichana huyo mdogo ampate huyo mwanasesere, maana alikuwa ameomba sana maskini huyo mwanasesere. Kwa hiyo alitoka akaenda na kumnunulia mwanasesere wa nguo, kitu ki—kidogo, labda yapata senti thelathini; kitu kidogo kichafu alichokuwa amenunua, chini kando ya barabara. Na ulikuwa ni usiku wenye baridi sana, dho—dho—dhoruba kali za theluji zikivuma, theluji zikianguka pale kwa nguvu; na New York, moja kwa moja kwenye pwani.

117 Na mitaa ikijaa; na watu katika motokaa zao kubwa, za limosini. Na karamu za ulevi, nje wakilewa, sherehe ya kuzaliwa kwa Kristo na za mambo haya tunayozungumzia usiku wa leo, wakijaribu kuwazia kwamba hiyo ndiyo njia nzuri ya kuifanya; kulewa tu ili kusahau masikitiko yao na kadhalika, na hiyo—hiyo ndiyo njia ya kuifanya. Hao wote. . .

118 Nikisimama kwenye duka, hivi majuzi, na mwanamke fulani akizungumza kuhusu kile. . . wasichana wawili walikutana na walitaka kujua kile walichomnunulia baba yao. Ndipo mmoja wao akasema, "Vema, yeye. . . " Alimnunulia katoni ya aina fulani ya sigara. Na huyo mwingine akasema alimnunulia kisaga cha wiski na ninii—na ninii—na jozi ya karata. Sasa kama huko si kutoa zawadi ya kumbukumbu kwa kuzaliwa kwa Yesu Kristo! Na hivyo ndivyo inavyoenenda, mnaona, ni lundo kubwa la mapambo. Haina Krismasi ndani yake hata kidogo.

119 Na kwa hiyo basi tunapata sasa, maskini mtu huyu, alichanganyikiwa. Naye alijua moyoni mwake kwamba maskini msichana wake alikuwa ameondoka, bali alienda na kununua mwanasesere hata hivyo. Ndipo akawaza, "Nitaanza tu kutembea, nitampata mahali fulani. Atakuwa mtaani hapa nami nitampata." Ndipo akaanza kutembea.

120 A—asingeweza kujipumbaza, msichana huyo hakuwepo kule kwenye kibanda na katika maskini kijitanda kibovu, kichafu; bali, alizikwa. Kwa hiyo, a—alijua. Alidhani angemkuta mtaani. Akasema, "Nitaendelea tu kutembea." Basi alikuwa akiteremka kwenye vichochoro, wakati wao wakiimba nyimbo zao za Krismasi na kuendelea. Na akiteremka vichochoroni, huku amebeba huyu mwanasesere mdogo, mchafu; amemshikilia kwenye koti lake, juu moyoni mwake, akiwazia maskini msichana wake.

121 Basi hatimaye ilitokea kwamba polisi alimwona, naye polisi huyo alikuwa na vinywaji vichache mwenyewe, ndipo akakimbia kuingia kichochoroni na kumshika mzee huyo na kumgeuza. Akasema, "Unafanya nini kuzurura hapa ndani?"

122 Akasema, "Ninampelekea maskini mwanasesere huyu, bwana, binti yangu mdogo."

123 Akasema, "Vema, unaishi wapi?" Naye akamwambia mahali alikoishi. Akasema, "Vema, unaenda mbali na huko, umelewa. Rudia ile njia nyingine."

124 Kasema, "Bwana, si—sijalewa. Nilimwahidi maskini binti yangu ninge—ningemnunulia zawadi ya Krismasi." Tena kasema, "Zawadi impasayo msichana mdogo ni maskini mwanasesere."

125 Naye akasema, "Hebu nimwone." Kwa hiyo akamwonyesha maskini mwanasesere, wa matambara, aliyeonekana mchafu. Naye alikuwa amemshikilia kwenye ninii yake. . .karibu na kifua chake, akishikilia maskini mwanasesere wakati yeye. . . Kwa hiyo polisi huyo, amelewa nusu, mwenyewe, akamsukuma na kuanza kuteremka. Mzee huyo akateremka kichochoroni, huku theluji ikianguka upesi.

126 Basi, vema, karamu za usiku wa manane zikaanza. Kesho yake asubuhi, theluji ilikuwa imeisha, jua lilikuwa limechomoza. Na kwa hiyo wao bila shaka. . .watu wote kutoka kwenye karamu zao za maadhimisho walikuwa. . .mifuko ya barafu vichwani mwao, kutokana na kunywa kupindukia na sherehe ya ku—kuzaliwa kwa Kristo. Pia—pia wengi wao walikuwa wamepwelewa na sauti kutokana na kufanya yasiyofaa, kutokana na shughuli zote.

127 Lakini kule chini kichochoroni, walimpata mzee huyo. Ndipo walipomgeuza, alikuwa na maskini mwanasesere huyo karibu na moyo wake. Nadhani alimpelekea yule msichana zawadi yake. Alimpata katika Nchi isiyo hapa. A—a—alipeleka zawadi hiyo. Ilikuwa ni zawadi ifaayo. (Mungu, mwenye rehema.) Hata hivyo ilimgharimu kifo chake. Hamna njia yoyote nyingine ulimwenguni angaliweza kumpa msichana huyo zawadi hiyo, msichana alikuwa amezikwa. Ila njia pekee angaliweza kufanya hivyo, ingalikuwa ni kwenda namna hiyo. Maskini mwanasesere huyo hakuwa na maana sana, nadhani, maskini mwanasesere mwenye uso mchafu, lakini alininii . . . alimfanyia nini? Alitimiza ahadi aliyokuwa ametoa. Haijalishi kile watu walichowazia juu yake, mikono yake michafu juu ya maskini mwanasesere, mchafu, bali i—ilitimiza ahadi kwa maskini msichana wake.

128 Wakati mwingine wanaiangalia Injili kama kuimba, kucheza, hawakutaka Hiyo wakati Mungu alipoileta, lakini ilitimiza ahadi kwamba Yeye angalimtoa Mwana Wake. Basi mnajua nini? Walimwacha afe, pia, kama tu vile mzururaji mtaani. Hiyo ni kweli kabisa, wamemwacha Yeye afe kama tu vile mzururaji mtaani. Na leo hii wanamtendea Yeye kama mzururaji mtaani, lakini Yeye alitimiza kile Yeye alichopaswa kufanya. Alikuwa ndiye Zawadi ambayo Mungu aliahidi kwa ulimwengu.

129 Usiku wa leo, hebu nimchukue Yeye kama Mwokozi wangu kwa moyo *wangu*. Hebu nitembee usoni pa kifo changu, ama chochote kile, namna hiyo. Niliahidi maisha yangu Kwake. Ninataka kuyapeleka Kwake. Haijalishi kinachonibidi kupitia, kama inanibidi kupitia mauti, kama inanibidi kupigwa risasi; haijalishi kinachotendeka, inanibidi kuchekwa, kuitwa "mwendawazimu," kila kitu, kutengwa na makanisa mengine yote ya Wakristo na kadhalika, mimi. . .ni karama ya Mungu ninayoshikilia moyoni mwangu. Aliitoa, ninataka kuipeleka Kwake.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

130 Zawadi zifaazo ninazungumzia, ilikuwa ni zawadi iliyofaa kwa sababu maskini msichana. . .alikuwa ni msichana mdogo, kuwa, maskini mama (angalikuwa), zawadi ifaayo ilikuwa ni mwanasesere mdogo. Zawadi ifaayo ambayo Mungu, Muumba, angeweza kuyapa maumbile Yake, ingekuwa ni Mwokozi kuyaokoa kutoka katika hali yaliyokuwa. Sijui, usiku wa leo, tunapokaribia Krismasi sasa, nami nadhani itakuwa ndio ujumbe wa mwisho tunaosikia kati ya sasa na Krismasi, 'sipokuwa tupate ujumbe wa redio wa mtu fulani.

131 Nashangaa, usiku wa leo, kama tumekubali Karama ambayo Mungu alituahidi: Uzima wa Milele, kumwamini Kristo na kupokea Roho Mtakatifu. Kama hujafanya hivyo, ungependa kuikubali karama ya Mungu ya Krismasi, iliyo halisi na kweli, je! waweza kuinua mkono wako? Sema, "Ndugu Branham, si—sijui, wa—wakati mwingine nimeamini Hiyo. Nami nimeangalia mambo ninayofanya. Na kwa namna fulani, kidogo, nina shaka." Msi—msiwe na shaka tena, enyi rafiki.

132 Mnaona, ku—kumechelewa sana kuwa na shaka sasa. Hebu tuwe na hakika sana na hiyo. Sema, "Niombee, Ndugu Branham, na ninataka ku. . .Karama ya Mungu kwa ulimwengu, ni Yesu Kristo. Ni—ni—ninataka hii iwe Krismasi halisi. Ninamkubali Roho Mtakatifu moyoni mwangu. Hiyo ingeweza kunishikilia kupitia dhoruba zote za maisha, ndipo siku moja ninaweza kuja katika Uwepo Wake pamoja na karama hii ya Uzima wa Milele. Atanikubali juu ya misingi hiyo, hiyo ndiyo njia pekee Yeye ataifanya."

133 Ama, je! unayo zawadi ifaayo usiku wa leo? Aina ya mtazamo ufaao? "Baba, nitakufuata Wewe popote uendapo. Lolote Wewe usemalo, 'Fanya,' nitalifanya. Lolote Neno Lako lisemalo kwangu, 'Fanya,' nitalifanya. Naam, Bwana, sijali yale watu wengine wote wasemayo, nitalifanya kwa sababu ninaitaka Karama Yako; ni Uzima, na Kristo ni Neno."

134 Ikiwa huwezi kuamini Neno lote, na useme, "Vema, sijui, ni—ninaamini kwamba. . .*hili*, ninaamini *lile*, bali siwezi kabisa kwenda *hili*, siwezi kwenda *lile*." Wewe ni kama wale sabini walioondoka. Hawawezi kukubali Neno lote na kumpokea

Kristo katika utimilifu wa Uungu Wake na huduma Yake; na tayari kufa kama Yeye alivyokufa kwa ajili yako.

135 Basi waweza tu kuinua mkono wako, huku umeinamisha kichwa chako, na useme, "Niombee"? Mungu akubariki. Na Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, msichana mdogo. Loo, Mungu akubariki. Naam, ninauona mkono wako. Bwana akubariki, hakika. Karama hii ndogo, ya Kristo, ambayo Mungu aliitumia ulimwengu; na kuitambulisha kwa...Mamajusi aliitambulisha, maisha Yake Mwenyewe yakatambulisha Hiyo, kifo Chake kikatambulisha Hiyo, kufufuka Kwake kukatambulisha Hiyo, kukubali kwako kukatambulisha Hiyo, na Yeye anajitambulisha Mwenyewe na wewe kwamba wewe ni Wake na Yeye ni wako. Ikiwa kwa kweli wewe si...unaona, tendo la Roho wa Mungu akifanya kazi ndani yako, katika majira haya ya Krismasi, naomba likujie sasa.

136 Baba wa Mbinguni, tunapoyumbayumba kama mzururaji mtaani, hakuna mtu aliyekuwa na haja naye hata kidogo. Ulimwengu uliendelea moja kwa moja katika karamu zao za kipumbavu, ndivyo walivyo usiku wa leo, Bwana. Lakini wakati mwingine tunajisikia kama yule mzururaji, ila tumeikubali Karama. Kwa hiyo tunaomba, Baba, kwamba utatufanya sisi karama, ya nuru, kwa ulimwengu huu unaokufa. Wengi hapa wameinua mikono yao kwamba wanaitaka Karama ya Mungu ambayo ilimbidi Yeye, Mwenyewe, kumtoa Mwana Wake wa pekee, akashuka chini, akawa Mtu. Alijishusha sana hata hawakuninii...Alijishusha sana na kuwa mnyenyekevu sana hata Ha—Hakuwa hata na kitanda cha kuzaliwa ndani. I—i—ilibidi ng'ombe a...ama farasi au kitu fulani ilibidi kuachilia hori lake, asimame kando, (mnyama) wanadamu walikuwa wameingia sana katika hali iliyokuwepo. Yeye—Yeye akashuka chini kwenye—kwenye hori, zizi dogo la pangoni kwenye ubavu wa kilima huko Bethlehemu, ambapo mwana wa kahaba alikuwa ameanzisha mji mdogo miaka mingi hapo kabla.

137 Na sasa, Bwana, tunapata kwamba usiku mmoja, usiku wenye baridi, aliambiwa, "Rabi, tunataka kwenda na Wewe nyumbani usiku wa leo."

138 Ndipo Yeye akasema, "Vema, sasa, ndege wana viota, na—na mbweha wana mapango, bali mimi—mimi—mimi sina... hata mahali pa kukiweka kichwa Changu." Na hivyo ndivyo walivyomwacha Yeye kufa, kama mzururaji mtaani.

139 Baba wa Mbinguni, hivi M—Mkristo, hivi watu leo hii wanaweza kuona kwamba—kwamba Hiyo ndiyo ile Karama kuu? Na wengi hapa, usiku wa leo, zaidi ya dazani moja, nadhani, waliinua mikono yao kwamba walitaka kumpokea Roho Mtakatifu. Naomba kama tu wale mamajusi, huenda hakuna hata mmoja kwenye kusanyiko atakayeona hata kile

kinachoendelea. Na hii Nyota, Nuru hii ya ajabu ilipita juu ya mahali pa kuangalilia nyota, kwa miaka miwili, ambapo watu hata walijua saa wakati huo kwa saa nne, walijua saa kwa nyota. Hakuna mtu, hakuna mwanahistoria aliyeandika kuhusu hiyo. Hakuna mtu aliyejua chochote kuhusu Hiyo, na hata hivyo Hiyo ilikuwepo. Na hawa mamajusi, wakiwa na zawadi yao ifaayo, waliongozwa moja kwa moja kufikia Hiyo. Jalia Nuru iyo hiyo ije katika kila moyo, hapa usiku wa leo, wanaoketi hapa. Huenda kusiwe na msisimko wowote, huenda kusiwe na *hili*, *lile*, na labda hakuna mtu mwingine angejua hilo, kama tu wale mamajusi. Lakini jalia jambo fulani likolee sana katika mioyo ya hawa wanaume, wanawake, wavulana na wasichana usiku wa leo, kwamba Karama hiyo ya Mungu itatia upako maisha yao. Kwamba kuanzia usiku huu na kuendelea, watabadilishwa. Hawatakuwa tena jinsi walivyokuwa. Watakuwa ni ki—kiumbe kilichobadilishwa tangu sasa na kuendelea. Wajalie, kama wale mamajusi, wageuke na wasirudi kwenye mitindo ya ulimwengu (naye Herode, ikulu ya mfalme), "Bali wakionywa na Mungu, walienda kando." Tujalie, Bwana.

140 Usiku wa leo ninaomba ya kwamba kila mwanamume mwenye busara, mvulana, au msichana, hapa ndani usiku wa leo . . . Mwanamume ama mwanamke aliye na busara ya kutosha kugeuka kutoka kwa mambo ya ulimwengu usiku wa leo, asirudi nyuma tena baada ya siku hii. Baada ya huku—huku kupita kwa mchana huu na usiku, hawatarudi tena katika mambo ya ulimwengu, lakini wajalie wawe na busara. Nayo Sauti hii ndogo ya ajabu iliyowafanya kuinua mkono wao na kusema, "Naam, ninataka Karama ya Mungu . . ." Jalia jambo lilo hilo lililowafanya kuinua mkono wao, liwatambulishe usiku wa leo na mauti Yake, kuzikwa, na kufufuka, kwa kuwapa Roho Mtakatifu. Jalia wageuke.

141 Wajalie wanawake hawa usiku wa leo, Bwana, ambao wamekuwa na wakati mgumu kujizuia wasiambatane na ulimwengu; waache nywele zao zikue, na kuvalia kama wanawake, na kuondoa hivi vipodozi na kadhalika, hivi vitu bandia, vinavyoonyesha . . . hivyo—hivyo kwa namna fulani vinawatambulisha kuwa hawana afya njema, wao . . . kuna—kuna kasoro fulani. Pia jalia usiku wa leo, Nuru hii ndogo ya ajabu, Bwana, iliyowafanya kuinua mikono yao, jalia waseme, "Bwana, ninageuka kuyaacha mambo ya ulimwengu, usiku wa leo."

142 Watu hawa ambao hawajakuwa na ki—ki—kitu fulani halisi, ambacho kingezungumza na wake zao na kuwafanya kugeuka; na mambo wafanyayo. Jalia sisi sote kwa pamoja, Bwana, tugeuke tu usiku wa leo, tukionywa na Mungu kwa ujumbe huu mdogo wa ajabu wa Nu—Nuru ya Mungu inayomulika juu ya mioyo yetu. Tujalie tugeuke usiku wa leo na—na kuishi kwa ajili Yako siku zetu zote, twende—twende nyumbani pamoja na Wewe

kwa njia nyingine mbali na ile ambayo tumekuwa tukisafiria. Tujalie, Bwana. Tufanye Wakristo bora, kila Mkristo hapa usiku wa leo, Baba, ambaye amekukubali Wewe na anakuamini Wewe. Nao wamejaribu kuishi maisha ya Kikristo, lakini usiku wa leo, jalia wageuke, jalia wapokee Karama hiyo.

143 Ee Mungu, ni—ni ninii—ni njia iliyodharauliwa. Wanawake wataitwa "wa mtindo wa kale," wataitwa kila kitu. Nao wanaume wataitwa "walokole." Lakini sisi—sisi tuko tayari, Bwana.

144 Roho Mtakatifu, tugeuze, sasa hivi. Nigeuze, Bwana. Si—si—sitaki hata kuenda njia yoyote ambayo ingeweza kunipeleka mbali na Wewe. Bwana, ni—ninataka tu kuenda jinsi ambavyo Wewe ungenitaka niende. Ninataka karama ya moyo wangu iwe kamilifu sana hata itakutambulisha Wewe, Bwana, duniani, kwamba Wewe hujafa, U hai.

145 Wewe ni Mungu wa walio hai, si Mungu wa wafu. Aliyekufa amejawa kila mahali na nzi, na nzi wa chooni, wakileta vijidudu na nzi wengine wa chooni; kama mtu anayekunywa kwa mara yake ya kwanza, anayevuta sigara yake ya kwanza, anayesema uongo wake wa kwanza, anayeenda nje akimwacha mkewe kwa mara ya kwanza; ama mke anayeenda nje akimwacha mumewe, ama kufanya mambo yasiyofaa; kama tu vile nzi wa chooni amewaangukia, naye. . . wa—wanaongezeka kwa ninii. . . wanaenda kwenye vyoo na kinyaa, kwa sababu ni kwenye nafsi iliyokufa ndani. Roho chafu zinajitoma ndani yake. Na roho moja chafu inaweza kumsababisha kufanya kitu kingine; na nyingine inakuja, imsababishe kufanya jambo jingine kwa sababu zilifanya *hili*.

146 Mungu, jalia wageuke na kujia Uzima. Jalia wainuke, na Malaika wa Mungu washuke pamoja na vipawa vya Uzima wa Milele, Bwana, na waenende kutoka utukufu hadi utukufu. Tujalie, Baba. Tunageuka, usiku wa leo, kutoka kwa mambo ya ulimwengu na mahangaiko ya ulimwengu, tukionywa na Mungu kwamba wakati umewadia, Yesu anarudi duniani. Pia jalia Roho Mtakatifu Mkuu atupatie, usiku wa leo, ule Uzima wa Milele tunaoutafuta. Tujalie, Bwana. Sisi—sisi tunaomba tu kwamba Wewe utatujalia baraka hizi kwa kuwa tumeomba hayo katika Jina la Yesu Kristo.

Huku tumeinamisha vichwa vyetu:

147 Mamajusi zamani za kale walikuja kwenye ile. . . walifuata ile Nuru hadi kwenye. . . waliipata Nuru Kamilifu. Pia naomba Nuru hiyo ndogo, usiku wa leo, iliyokufanya kuinua mkono wako, ama labda hata hukuninii. . . Hiyo ilikuangazia, bali hata hukuinua mkono wako, naomba Nuru hiyo ikuongoze moja kwa moja hadi kwenye ile Nuru Kamilifu.

Hebu na tusimame tu sote, kwa ajili ya ibada fupi ya kujiweka wakfu.

148 Naomba tuufanye maskini moyo wetu hapa, usiku wa leo, makazi ya Kristo. Kumbukeni, usiku wa leo, maskini hadithi yangu fupi ya ajabu kuhusu yule mzururaji. Usiku wa leo, kwa kweli, Yesu Kristo ndiye huyo mzururaji mtaani. Hiyo ni kweli, Yeye—Yeye alikuwa ni mzururaji mtaani. Loo, naam, tunasema, “Tunamtumikia Yeye.” Hakika. Mapambo yote na madoido, hayo si Yeye. Hayo si Yeye. Ilimbidi kufa kukuletea Karama hii, si mwanasesere, bali Uzima. Ilimbidi kufa ili kufanya hivyo, kukufikia, njia ya pekee ambayo Yeye aliweza kukufikia. Asingeweza tu kuja hapa na kuwa Mtu mkamilifu, kama Yeye alivyokuwa, na kukufikia. Asingeweza kulifanya kwa njia hiyo. Ilimbidi kufa ili kufanya hivyo, kuleta—kukuletea Karama ya Mungu. Kama vile m—mzururaji ilimbidi kufa ili kumfikisha yule maskini mwanasesere kwa msichana wake, Kristo ilibidi afe ili kukuletea Mungu. Tunataka kukubali Hiyo usiku wa leo. Nami ninaamini, huku vichwa vyetu vimeinamishwa,. . . basi hebu tumwinulie tu Mungu mikono yetu na kuweka wakfu maisha yetu upya, papa hapa usiku wa leo.

149 Ee Mungu mwenye Rehema, sisi—sisi tunataka Karama Yako. Ni—nipo hapa, kama majira haya ya Krismasi, Bwana, ninapotambua na kutazama juu ya nchi na kuona mapambo na madoido ya siku hii, ni—ninaweza tu kuona ninii . . . kule nje, kama Biblia ilivyosema, wakati huu wa Laodikia, Wewe uko nje ya kanisa Lako. Umekataliwa, mtoro kwa kanisa Lako Mwenyewe na kwa watu Wako Mwenyewe. Wewe—Wewe—Wewe umekataliwa. M—mtoro ukiwa kitu kilichokataliwa, na Wewe umekataliwa katika kanisa Lako Mwenyewe. Umekataliwa miongoni mwa watu Wako. Hawakutaki, Bwana, nao wamekuacha Wewe, kama yule mzururaji, mtaani. Mungu, Wewe—Wewe—Wewe uliendelea, ukafa hata hivyo, ili uweze kutuletea sisi Karama ya Mungu. Nasi kwa unyenyekevu tunaikubali Hiyo, Bwana. Ninaomba kwamba Wewe utaijaza tu mioyo na maisha yetu. Na kutugeuza, tangu usiku huu na kuendelea, na jalia tuwe Wako kabisa tunapojiweka wakfu Kwako.

150 Nipokee, Bwana. Makosa ya maisha ni mengi ambayo nimefanya. Na, mpendwa Mungu, wa—wa—wakati ninaposimama hapa juu ya mahali hapa patakatifu ambapo Injili imehubiriwa na ambapo tumekuona Wewe hapa, hata katika Nu—Nuru kuu iliyoangaza juu yao. Pia tuna shukrani sana kwa hili, Bwana. Na—najiweka wakfu kwa ajili ya Krismasi hii, si katika . . . na kama ulimwengu ungefanya ama ku—ama kufungua kurasa mpya. Bwana, ni—ninataka tu kumkubali Mwana Wako. Ni—ninataka kuikubali Karama Yako, Bwana.

151 Ninataka kuikubali Karama ya Uzima wa Milele kupitia Kristo. Na mimi, kwa kweli, Bwana, ninaikubali Karama ya Kristo kwangu, kujaribu kuwaleta wengine Kwako. Mungu, sisi kila mmoja . . .

152 Mfanye maskini mke wa nyumbani kuwa mwema sana na mnyenyekevu, hata ataweza kuwaleta wengine Kwako. Karama ambayo Wewe ulimpa, maskini sifa hiyo ya kike ya umama, jalia awe na sifa ya mama sana hata majirani watamwona na—na kutamani kuwa kama yeye.

153 Mfanye mwanamume huyo, mfanyakazi dukani, yeyote yule, Bwana; mpe maisha manyenyekevu, kama Kristo, ili wengine waweze kuona. Hatujui mahali watu hao wamesimama huko nje, Baba, bali hatutaki kuiacha ile barabara kuu, ya kale; bali tutaegemea nyuma, tuegemee mbele, tunyoshe mikono popote ili kupata nafsi. Iweke hiyo mahali tunapoweza kuifikia, Bwana, tunaomba. Na utupatie ma—ma—maisha ambayo yangeweza kufanya watu watamani kuishi namna hiyo, tunapojiweka wakfu Kwako, usiku wa leo. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa, kama mtainamisha vichwa vyenu tena, ninataka kuombea kila mmoja wenu heri za Krismasi:

154 Naomba Karama kuu ya Krismasi, Ile ya kwanza na ya pekee na ya asili na Ya pekee iliyopo, Yesu Kristo, iwe mpya moyoni mwako usiku wa leo. Hebu Roho Mtakatifu aje kwenu na awaletee karama za huduma na kadhalika kutoka kwa Mungu, hata nyinyi . . . karama ili uweze kuishi maisha yaliyo bora. Hayo ndiyo nitakayo. Afadhali niwe na Uzima wa Kristo ndani yangu kuishi maisha mema na ya ushindi kuliko vile ningetamani karama zote za uponyaji, karama za unabii, karama zingine zote; nipe tu Yesu. Jalia niishi Maisha, Maisha ndiyo ninayotaka kuishi. Ninataka kuishi kusudi wengine wajue. Hiyo ndiyo ninii yangu—hiyo ndiyo shauku yangu kwenye Krismasi, na ninaomba hiyo ndiyo shauku yako. Pia ninaomba kwamba Mungu atatupa shauku Yake.

155 Sasa, hebu tupate neno kutoka kwa mchungaji, na kuturuhusu tuondoke. Basi Mungu awabariki. Tutawaoneni Jumatano usiku. Hadi wakati huo, Mungu awabariki.

Karama Za Mungu Daima Hupata Mahali Pao SWA63-1222
(God's Gifts Always Find Their Places)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 22 Desemba, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org